# Kujaribu Kumtumikia Mungu Bila Ya Kuwa Ni Mapenzi Yake

Shreveport, Louisiana USA
Novemba 27, 1965B

1 Ndugu wahudumu, nanyi marafiki huko nje, nasema ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo. Utangulizi kama huo, mbona, sijui jinsi gani nitaishi kulingana na huo.

Lakini nikiketi tu pale tukizungumza, mimi na Ndugu Noel, siamini nimewahi kukutana na mtu hasa … Sisi sote tumeumbwa tofauti, bali na Mungu yeye yule. Kama vile Ndugu Jack Moore, hakika amekuwa … Ndugu Noel alikuwa tu akisema, "Tangu nimekuwa hapa pamoja naye …" Huyo ni mkwewe, na jinsi alivyojifunza kumpenda na kuheshimu hekima yake na kadhalika. Na hiyo … Ninaweza kusema "amina" kwa hilo. Mambo mengi mazuri … nyakati ambazo tumekuwa pamoja, yeye na mimi, na Ndugu Brown, Ndugu Boutliere hapa. Watu wema wa Mungu ambao kweli ninawapenda kwa moyo wangu wote.

Na sasa ni—ni ninaona hatuwi vijana kamwe, ama nafikiria tu juu ya wakati sasa ambapo tunajiona tunapobadilika tangu yapata miaka ishirini iliyopita tulipokuwa tukivuka majangwa, na kadhalika pamoja kama vijana. Lakini kujua tu kwamba kuna Nchi ambayo hatutazeeka kamwe. Tutakutana kule tena siku moja.

2 Jana usiku nilipokuwa nikiondoka kwenye Maskani, kulikuwako na maskini bibi mdogo aliyekuwa amelala pale kitandani, naye akasema, "Ndugu Branham, miaka mingi iliyopita …" Nafikiri alikuwa amepooza. Akasema, "Uliniambia …" Ninasahau yale matamshi ya mwanamke huyo yalivyokuwa sasa, kitu kama hiki, ninatumaini ya kwamba sitalinukuu vibaya. Kasema, "Kwamba mateso haya niliyokuwa nayo yangekuwa kwa kusudi fulani," ama kitu fulani, kwamba angepata mtoto. Naye hangeweza kuelewa jinsi hilo lingefanywa na yeye akiwa katika hali hiyo.

Pale alisimama kijana mwanamume, mwenye sura nzuri, akasema, "Mimi ndiye mtoto mchanga aliyemzaa." Kasema, "Mimi ndiye mtoto mchanga aliyemzaa."

Na mambo mengi sana yametukia njiani, hata hatuna wakati hapa wa kuyazungumzia. Tutafanya hivyo upande wa pili.

3 Na Tawi hili la Wafanyi Biashara. Mimi si mfuasi wa dhehebu lolote, nadhani kama nyote mjuavyo, bali mimi … Hili ndilo kundi pekee ambalo nimeunganishwa nalo, kubeba kadi ya ushirika, ni … Wao ni wa madhehebu mbalimbali, ni wafanyabiashara tu. Wamekuwa rasilimali kuu sana kwangu na kwa huduma ambayo Bwana Baba yetu amenipa mimi. Ni…si kwamba mimi sipendi madhehebu; ni huduma tu ambayo nimepewa, na kama mimi si mwaminifu kwa wito huo, basi nitakuwa mtu asiye mwaminifu kwa Mungu.

4 Na, ninawazia, kabla tu sijaondoka Tucson, labda wengi wenu mlikuwa kule, siku moja nilikuwa, Los Angeles nikizungumza na tawi hili. Na kulikuwa na … Ndiyo kwanza niyakemee madhehebu labda sana—sana. Si—sikukusudia kuwa hivyo. Kama unamaanisha hilo liwe duni, basi ningekuwa mnafiki. Haikupasi kufanya hivyo, la, hilo ni kumtupia tu mtu mwingine. Lakini nilikuwa nimesema juu ya mti niliouona katika yadi ya Ndugu Sharrit. Ulikuwa na aina kama tano za matunda juu yake. Nami nikasema, "Sijawahi kuona mti kama huo maishani mwangu." Ulikuwa ni … ulikuwa na balungi, ulikuwa na malimau, ulikuwa na chenza, kangaja, machungwa, kila kitu kikikua kwenye mti ule ule. "Vema," nikasema, "mimi—mimi hakika sielewi jambo hilo. Ni mti wa aina gani?"

"Ni mchungwa."

Nami nikasema, "Vema, huo ni balungi?"

Kasema, "Naam."

Ni—nikasema, "Inawezekanaje?"

Kasema, "Huo umepandikizwa."

Nami nikasema, "Loo, ninaona."

Akasema, "Yote ni jamii ya mchungwa, na mti wo wote ulio wa jamii ya mchungwa unaweza… unaweza kupandikizwa."

Nikasema, "Nafahamu." Ndipo nikaanza kupaza sauti kidogo tu, mwajua, maana nina wasiwasi na mhemko.

Kwa hiyo, akasema, "Kuna nini?"

5 Nami nikasema, "Vema, nilikuwa nikiwazia tu jambo fulani." Nami nikasema, "Sasa nataka kukuuliza swali." Nikasema, "Sasa, mwaka ujao wakati wa kuchanua, hakutakuwako na machungwa, makangaja, mabalungi, malimau; kutatakuwako tu na machungwa kwa sababu huo ni mchungwa, sivyo?"

Akasema, "La, la. La, kila tawi huzaa kwa jinsi yake."

Kasema, "Sawa."

Kwa hiyo hilo bado lilikuwa linasikika zuri sana, kwa sababu mimi…mwajua mimi ni…bila shaka nina digrii kutoka Hartford na vyuo hivi vingine vyote, mwajua. Kwa hiyo—kwa hiyo mimi…ninaangalia viumbe, hayo ndiyo chuo kikuu kilicho bora kuliko vyote nilivyopata kuona bado, chuo kikuu cha Muumba. Kwa hiyo kama nikiangalia jambo hilo, ninapata mahubiri yangu kwa jinsi ninavyoona maumbile yakitenda.

Nami nikasema, "Vema, hilo linanifanya tu kujisikia vizuri sana."

Akasema, "Kuna nini?"

Nikasema, "Nilifikiria tu jambo fulani."

6 Kwa hiyo, siku hiyo, nilikuwa nikihubiri juu ya jambo hilo. Nami nikasema, "Sasa, unaona, wakati kanisa lilipoanza mara ya kwanza, ilikuwa … Yesu alisema …" Nilikuwa nikihubiri Yohana 15. "'Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi. Na kila tawi lisilozaa matunda litakatwa, litateketezwa.'"

Na mtu fulani yuko tu kooni mwangu akinikaba sana kwa ajili ya jambo hilo, kasema, "Unaona, nilifikiri kama kweli wakati mmoja ulikuwa umejazwa na Roho Mtakatifu na umeokolewa, ulisema, 'hawangeweza kuliepa jambo hilo.'"

"Hiyo ni kweli."

Akasema, "Na *hilo* je?"

Nikasema, "Sasa unazungumza juu ya somo tofauti. Yeye anazungumza juu ya kuzaa matunda pale, si Mzabibu; Yeye anazungumza juu ya kuzaa matunda, wala si Uzima. Akasema, 'Vema, kata tu mti huo upate kukua, uzae matunda.'"

Yeye alisema …

Nami nikasema, "Sasa, unaona, mti huu, ulipoanza, wote walikuwa Wakristo halisi wa Biblia. Ndipo likaja tawi lililoitwa la Kilutheri, Methodisti, Baptisti, Presbiteri: ndimu na mengineyo." Nami nikasema, "Unaona, unastawi kwa jina la Ukristo, bali … Unaishi kwa Mti huo, bali unazaa kwa namna yake ya kimadhehebu. Mnaona? Lakini," nikasema,"iwapo ule mti wa chungwa utawahi kutoa kiungo kingine chenyewe, utazaa machungwa kama ulivyokuwa hapo mwanzo."

7 Kulitokea kwamba, ameketi pale, kiongozi wa ninii kubwa … moja ya madhehebu yetu makubwa sana ya Kipentekoste. Sijui jinsi ya kulifanya ili kwamba kila mtu atafahamu ya kwamba si wazo langu kwamba —kwamba mimi nina—ninawapinga hao ndugu, dada; hilo ni kosa. Ninaeleweka vibaya sana, nami sijui ni kwa nini. Mnaona? Watu wanafikiri hata siamini katika watu kwenda kanisani. Hiyo ni maili milioni moja kutoka kwenye Kweli. "Hatuna budi kukusanyika pamoja, na zaidi sana tunapoona siku ikikaribia." Mnaona? Hatuna budi kukusanyika pamoja katika umoja. Huenda tusininii …

Kama niliishi katika mji fulani na hawakuwa na kitu kule ila…vema, kanisa fulani (sitaki kutaja jina lo lote), lakini kanisa lo lote tu, kama waliamini jambo moja tu, ya kwamba Yesu alikuwa ni Mungu, mengine yote si kweli, ningehudhuria kanisa hilo. Kama siwezi kupata mkate mzima, ni—nitachukua kipande. Mnaona? Nitaenda kusikiliza, kumwabudu Bwana, na kumwonyesha ya kwamba ninatekeleza sehemu yangu. Ninataka Yeye ajue kwamba niko hai. Mimi—mimi … ninataka kila mtu ajue niko upande gani. Ninakusanyika pamoja na Wakristo, na hapo namwabudu na—na kumtumikia Bwana.

8 Lakini ni vigumu sana, mimi … ilikuwa ikinisumbua sana, na ndipo nikaona kwamba hata Bwana wetu alifahamika vibaya katika mambo mengi sana. Angesema lo lote, nao wangeninii…angefahamika vibaya. Nadhani haina budi kuwa hivyo tu. Bali wale walio na hekima watafahamu. Mnaona? Biblia ilisema hivyo. Watalishika.

Kwa hiyo asubuhi ya leo wakati nikisema hivi … Nami nikasema, "Sasa, wao—wao wanaishi kwa jina la Ukristo, bali wanazaa matunda mabaya. Ina tunda la kimadhehebu. Wanaweka kitu, na wanaishi moja kwa moja na hicho, na wanaishi kwa Maisha yale yale."

9 Ni vile nilikuwa nikijaribu kusema jana usiku, kwamba roho hiyo inaweza kubatizwa katika Roho huyo na bado asiwe Mkristo. Mnaona? Unaishi moja kwa moja kutoka kwenye Uhai ule ule, bali matunda unayozaa yanaonyesha kile ulicho. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Wanaweza kufanya ishara zote, na kuwaombea wagonjwa, na kuwaponya wagonjwa, na kufungua macho, na kutoa pepo, na—na kufanya mambo haya yote, wakiishi moja kwa moja kutoka kwa Uhai ule ule ulioko mle ndani, bali bado ni limao. Mnaona? Hiyo ni kweli. "Matunda, unajulikana," Yesu alisema. Na kwa hiyo basi tunaona …

Na niliposhuka jukwaani, kiongozi huyu mkuu akasimama, akasema, "Yeye hakumaanisha jambo hilo." Yeye alisema, "Tunajua ya kwamba sote tumepandikizwa." Vema, hiyo ni kweli ya kwamba tumepandikizwa, kisiki kilichopandikizwa, hiyo ni kweli; bali si katika Mzabibu, uliopandikizwa. Kwa hiyo

basi akasema … akaanza kwa namna fulani ya—kwa namna fulani kunikemea kidogo.

10 Na kulikuwako na kijana mwanamume pale, nafikiri ni wa jamii ya wacheza sinema fulani. Jina lake ni Danny Henry, naye alikuwa mvulana wa Kibatisti. Vema, yeye alikuja jukwaani kunikumbatia, naye akasema, "Ndugu Branham, natumaini hili halisikiki la kukufuru, lakini" kasema "Ninaamini hiyo ingeweza kuwa karibu sura ya 23 ya Ufunuo."

Nami nikasema, "Asante."

Naye akaanza kusema jambo lingine naye akaanza kunena kwa lugha, mvulana wa Kibatisti. Na wakati alipofanya hivyo, kulikuwa na m—mwanamke kutoka hapa Louisiana, yeye alikuwa Mfaransa, kwa namna fulani mwanamke mkubwa sana, aliandika tafsiri yake.

Vema, basi kulikuwa na kijana mwingine aliyeketi hapa aliyekuwa Mfaransa, aliandika yale aliyosema. Walilinganisha maandishi hayo, na yote mawili yalikuwa sawa.

Na halafu mvulana mkubwa, mwenye nywele nyepesi amesimama huko nyuma kabisa, kwenye Mkahawa wa Clifton, akaja akitembea. Akasema, "Hebu nione maandishi hayo."

11 Ninataka kuona jinsi zilivyokuwa, na zote tatu zilikuwa sawa kwa tafsiri. Yeye alikuwa mkalimani wa Umoja wa Mataifa, mfasiri wa Kifaransa. Na yalisema hivi:

> *Kwa kuwa umechagua njia hii iliyo nyofu na nyembamba, njia iliyo ngumu, umefanya hivyo kwa hiari yako.*
>
> *Lakini ni uamuzi mzuri jinsi gani uliofanya, kwa sababu ni NJIA YANGU.*

Mnaona? Kisha akasema … na kuendelea na kusema basi:

> *Jambo hili lenyewe ndilo litakalotimiliza, na kufanya na kutimiliza, ule ushindi mkuu sana katika ule Upendo wa Kiungu.*

Mnaona, daima, hata katika Kifaransa, kitenzi mbele ya kielezi pale katika—katika—katika hiyo fasiri. Kwa hiyo katika jambo hilo nisingeweza kusema … Musa, alifanya chaguo lake, ilimbidi kufanya chaguo lake. Sote inatubidi kufanya uchaguzi wetu na kufanya vizuri tuwezavyo. Na Mungu … Ninaheshimu ujumbe wa mtu yeyote ambaye ametoa kuhusu Mungu. Mimi … cho chote kile, ninaheshimu hilo kwa moyo wangu wote.

12 Sasa, ninaona Ndugu fulani mdogo alikuja muda mfupi uliopita, Ndugu Stringer, nafikiri kutoka huko Louisiana … ama Mississippi, alituletea picha chache hapa ambazo mmetuona tukiziangalia. Ilikuwa ni ya Malaika wa Bwana, wakati alipotokea. Ni wangapi wameisikia hiyo hadithi? Nadhani kila mmoja wenu hapa amesikia. Mmekuwa nayo kwenye kanda, na kadhalika.

Sasa, niliambiwa hayo asubuhi moja kwenye saa nne, nikiwa nimesimama chumbani mwangu Indiana. Akaniambia nitakuwa Tucson, itakuwa ni wakati wa asubuhi na mapema, nitakuwa nikiondoa kichomanguo (tunavyoviita hapa, kichomanguo) kutoka kwenye mguu wa suruali yangu. Ndipo Malaika saba wakaja na kulipua hii, ndipo ardhi ikapasuka na kila kitu, kuninii…miamba ikabingirika kutoka milimani, na Malaika saba wakasimama pale.

Nami nikasema, "Vema …" Ndipo nikasema, "Vema…" Nilimwambia mke wangu, naye yuko mahali fulani hapa asubuhi ya leo, "Tayarisha kila kitu maana hakuna njia mwanadamu angaliweza kustahimili huo," nikasema, "atoke katika huo. Ninaenda Tucson, kazi yangu imekwisha hapa duniani. Ninaenda Nyumbani kuwa pamoja na Bwana Yesu."

"Vema," akasema, "una hakika?"

Nikasema, "Naam. Naam, hakuna mtu angeweza—angeweza kustahimili jambo hilo. Hakuna njia ya kufanya jambo hilo."

13 Nilihubiri tu zile *Nyakati Saba za Kanisa.* Hapo ndipo nilipokuwa nimemwita ndugu yetu hodari, Ndugu Jack Moore kumwuliza kuhusu hili, Yesu, katika Ufunuo 1, amesimama pale akiwa na nywele nyeupe na kila kitu.

Nikasema, "Yeye alikuwa kijana mwanamume." Na hapo ndipo ule ufunuo ulipokuja kwamba hiyo aliyovaa ilikuwa ni wigi, wala si Yeye; Yeye ana wigi (na mimi sikuwaweza kuelewa jambo hilo), kwamba ni Mungu Mkuu. Na majaji wa kale katika Israeli walifanya hivi, walipaswa wavae wigi nyeupe. Na ile nyeupe inamaanisha usafi. Nao majaji wa Kiingereza mpaka leo hii, katika mahakama kuu za Uingereza, wanavaa wigi nyeupe wakati wanapotoka, kwa sababu hakuna sheria nyingine juu ya sheria zao duniani. Mnaona? Nao ni majaji wakuu.

14 Nami ninakumbuka nilienda kule Arizona na kila kitu, ninajaribu niwezavyo … Niliogopa sana. Nilienda

kwenye mkutano wa Phoenix. Na kumbukeni, nilihubiri mahubiri, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Mnakumbuka hilo? Nilisema ya kwamba niliona jambo hilo, nikasema, "Kabla halijatukia, kumbuka, BWANA ASEMA HIVI, 'Jambo fulani litatukia.'" Labda mna kanda katika maktaba yenu ya kanda sasa. Na hapo nikasema, "Mnakumbuka sasa maono ambayo hayashindwi kamwe. 'Kitu fulani kitatendeka.' Kumbukeni!"

15 Na siku chache baada ya jambo hilo, nilikuwa na wasiwasi, na nikawaza, "Ni kitu gani hiki? Je! Nitakufa? Kama … Ninatumaini ni kitu cha haraka upesi ili nipate kukipitia. Sitaki kukawia."

Na asubuhi moja Bwana akasema, "Panda juu kwenye kilele cha Mlima wa Sabino."

Nami nilikuwa huko juu nikiinua mikono yangu, nikiomba. Nilisikia kitu fulani kikiupiga mkono wangu. Ulikuwa ni upanga. Sasa, unaweza tu kuwazia jinsi ungejisikia, ukisimama pale peke yako na hiki hapa kisu mkononi mwako urefu kama huo. Nikakichomoa na kukiangalia. Kilikuwa ni kisu tu, kimojawapo … nami ninaogopa kisu, hata hivyo. Nacho kilikuwa na—kilikuwa na chu—chuma, kitu kama moja ya visu hivi, kama chuma ama cho chote kile, kikali sana na chembamba. Kilikuwa katika na ala *hapa*, ambapo wale wanaopigana kwa panga wakinii, wakijihami wasikatane mikono, na—na kilikuwa na lulu kwenye mpini hapa. Kilienea tu mkononi mwangu vizuri sana. Vema, nilifuta uso wangu na kuangalia nyuma.

Mahali papo hapo, hivi majuzi, nikaona maskini hua mdogo akishuka. Nitawaambia habari zake badaye.

16 Basi nilikuwa nimeshika hicho mkononi mwangu, nikawaza, "Ajabu hii. Sasa, Bwana, mimi … ninachanganyikiwa? Hakuna mtu hapa. Mimi niko maili nyingi kutoka kwa mtu yeyote na huu hapa upanga. Nilikuwa nimeinua mikono yangu juu, na umetoka wapi?" Nami nikawaza, "Hilo ndilo jambo la ajabu sana. Sasa hebu angalia hapa, ni upanga; mnaona, niliugusa, na ulikuwa ni upanga." Nami nikasema, "Hakuna mtu hapa anayesimama hapa. Niko kwenye kilele cha miamba hii, moja kwa moja juu kabisa ya mlima." Wala hata usingeweza kuona Tucson kutoka mahali hapo, ilikuwa mbali sana huko chini.

17 Nikawaza, "Sasa, hilo ni jambo la ajabu. Sasa, haina budi katika mahali fulani hapa, yuko mtu fulani ambaye anaweza kuumba na kutengeneza upanga na kuuweka mkononi mwangu." Nikasema, "Inaweza tu kuwa ni Mungu yule yule aliyeumba kondoo dume kwa ajili ya Ibrahimu, angeweza kuwaumba hao kindi," ambao mmesikia. Basi nikasema, "Hivi hapa vitu, vitu vitatu mbalimbali ndani yake, nami ninaushika mkononi mwangu ukiwa halisi tu kama kitu cho chote kile ningaliweza kushika mkononi mwangu."

Nami nikasikia Sauti, ikasema, "Huo ni ule Upanga wa Mfalme!"

18 Ndipo nikawaza, "Sasa, Hilo lilitoka wapi? Nilikuwa papo hapo kwenye hiyo miamba mahali fulani." Nami nikainua mkono wangu namna *hiyo*, nikasema, "Upanga wa mfalme." Ndipo nikaangalia kote, na upanga ulikuwa umeondoka. Nami nikasema, "Upanga wa mfalme." Hiyo ni kuninii…wao hupandisha mashujaa cheo kwa—kwa upanga, nadhani hiyo ni kweli, jeshi ama kwa njia fulani, wanawapandisha cheo kwa huo. Basi nikasema, "Vema, labda huo ulikuwa wa kazi hiyo. Ina maana kwamba labda nitawekea wahudumu mikono, ama kitu kama hicho, kuwafanya wahudumu." Na halafu mimi …

Sauti ikanena tena, ikasema, "Upanga wa *Yule* Mfalme!" Si mfalme; Upanga wa *Yule* Mfalme! Mnaona?

Nikawaza, "Sasa, aidha mimi ninashikwa na kichaa, akili zangu zimefyatuka, ama kuna jambo fulani linalotukia, kuna mtu fulani amesimama hapa karibu na mimi."

19 Na ndugu, mambo haya ni kweli. Si—sijui jinsi ya kuwaambia, daima mmeona jambo hilo likitukia namna hiyo. Ni kweli. Mnaona? Na ni … Nisingeweza kufahamu jambo hilo. Kwa hiyo … Ni hisia ya ajabu sana.

Nami nikasimama pale. Nikawazia, "Sasa, ye yote yule ambaye amenizungumzia maishani mwangu mwote, tangu nilipokuwa mtoto mdogo, mdogo sana, amesimama papa hapa, nami siwezi kumwona kabisa." Nikasema, "Upanga wa *Yule* Mfalme?" Huo ungekuwa … Mungu ndiye *Yule* Mfalme. "Na upanga huu ni nini?"

"Neno, limewekwa mkononi mwako." Kasema, "Usiogope kufa, ni huduma yako."

20 Loo, jamani! Nilishuka kutoka kwenye mlima huo; kulia, kupiga mayowe, kwa sauti yangu yote, nikiruka juu ya miamba. Nikashuka nikaenda, nikamwambia mke wangu, nikasema, "Sitakufa, mnaona, ni—ni—ni huduma yangu." (Nilimwambia amwangalie Billy Paul hapa, na awachukue watoto. Nikasema, "Sasa, sina cho chote, lakini kanisa litahakikisha ya kwamba nyote hamkosi chakula na kadhalika, nami nita—nitakutana nanyi ng'ambo ya pili.") Na—naye … Nikasema, "La, sitakufa, ni jambo fulani kuhusu huduma yangu."

21 Siku chache baada ya hapo nilikuwa nikitoka kwenye mkutano; nilikuwa na telegramu ya kurasa tatu, iliyotoka hapa Houston, Texas. Na yule mtu aliyenikosoa sana usiku ule Malaika wa Bwana alipopigwa picha, picha Yake ilipopigwa kule Houston, alinipigia simu, akasema…alituma simu, mkewe akasema,

"Ninajua, Ndugu Branham, wewe una shughuli nyingi. Mwanangu, mvulana wa dada yake Ted Kipperman, anangojea kunyongwa kwenye kiti." Kasema … (vipi kama huyo alikuwa ni Billy Paul?). Akasema, "Yeye na msichana mdogo hawana budi kufa." Nanyi nyote mnalisoma kwenye gazeti, bila shaka. Kisha akasema, "Tumaini tulilo nalo tu ni wewe uje na kufanya mkutano na kuwakusanya watu pamoja."

22 Naye Raymond Huckstra tayari alikuwa ameniandikia mara nyingi, lakini unajua, nilikuwa nimepanga pale kwenye mkutano huo kwenda safari ya kuwinda pamoja na Bw. Mac Knelly na hao wengine. Basi nikawaza, "Vema, kama nikiwaacha hao watoto wafe na nisitie jitihada zangu, kamwe sitaweza kwenda kuwinda tena."

Kwa hiyo nikasema, "Vema, nitakuja." Nikaenda kule Houston, nikafanya mkutano, na bila shaka ninii… hawakuwaua, walininii tu…waliwaacha huru. Na hivyo ndivyo waivyotaka wafanye, kuwaachilia tu. Kwa hiyo hiyo ni kama miaka ishirini na moja, nadhani, huko—huko Texas.

23 Kwa hiyo basi, na nikirudi, nilipanda kwenda mlimani na niliambatana na Ndugu Fred Sothmann. Yuko hapa mahali fulani. Ndugu Fred, uko wapi? Papa hapa. Ndugu Fred Sothmann, Ndugu Gene Norman; siku moja, tulipokuwa kule siku ya pili, Malaika wa Bwana alishuka moja kwa moja kambini mahali tulipokuwa, na kuanza kunena juu ya watoto wao na mambo yale waliyokuwa wanafanya.

Niliondoka nikarudi kilimani. Nami tayari nilikuwa nimempata nguruwe wangu mwitu, na nilikuwa nikijaribu kumfukuza mmoja kumwelekeza kwa Ndugu Fred. Kwa hiyo nikapata mahali walipokuwa wakila kando ya kilima, na nikasema, "Vema, sasa, nitakwambia nitakalofanya, Ndugu Fred." Nikasema, "Sasa, wewe uende mahali pale asubuhi." Tunaenda kule mchana, tupande mlima. "Basi uende kule mchana, mimi nitaenda upande wa pili. Sasa, sitampiga risasi mmoja, lakini kama wakikimbia upande huu, nitapiga risasi mbele yao na kuwarudisha nyuma. Basi chagua aliye mkubwa."

"Vema," akasema.

24 Kwa hiyo Ndugu Fred akaenda kule. Na Ndugu Gene Norman (sidhani Ndugu Gene alikuja, sivyo?), Yeye alikuwa—alikuwa upande ule mwingine. Wengi wenu mnamjua Gene Norman, rafiki msiri wa wengi, ndugu mzuri. Naye akashuka chini kidogo. Ambapo, hao nguruwe, hawakuwapo tu asubuhi hiyo. Nami ningeweza kumwona Ndugu Fred, nikimpungia mkono, alikuwa karibu maili moja kutoka kwangu. Vema, nikawaza, "Hivi wangekuwa wameenda wapi?" Nilishuka nikaingia kwenye bonde kubwa, kisha nikashuka, nikawaza, "Nitaona kama ninaweza kuona mahali walipo." Nikaanza kurudi nyuma. Ilikuwa ni baada tu ya mapambazuko, jua lilikuwa limeanza kuchomoza.

25 Basi nikazunguka genge kubwa mno, loo, jamani, mamia na mamia ya futi, miamba mikubwa tu katika lile genge kuu kule, hizo kuta kubwa. Na ilikuwa kwa namna fulani inakuwa…jua lilikuwa linachomoza, kama saa moja, nadhani, ama kitu kama hicho. Basi nikaketi na nilikuwa nikiangalia huku na huko, ikatokea ya kwamba niliangalia kwenye mguu wa suruali yangu na hiyo hapo kishonanguo, mbegu yenye manyoya, manyoyanyoya. Nami nikasema, "Unajua, hilo laonekana ni la ajabu. Mnajua, Malaika wa Bwana aliniambia ningekuwa kama maili arobaini kaskazini-mashariki mwa Tucson, nitakuwa nikiondoa mbegu ya kishonanguo kutoka kwenye mguu wa suruali yangu." Mnakumbuka jambo hilo? Sivyo? Naam, bwana. Mnaona? Nikasema, "Hilo ni jambo la ajabu." Nilikuwa nimeshika mbegu hiyo.

26 Na mara tu nilipoangalia juu, niliona kama nguruwe ishirini hivi wakiwa kama yadi mia tano kutokea kwangu, wakatoka wakila majani haya ya faila kisha wakalala. Nikasema, "Sasa, kama ninaweza tu kumpata Ndugu Fred na kumpeleka mahali pale, atampata nguruwe wake papo hapo. Lakini najua yuko karibu maili moja ama mbili kutoka kwangu sasa. Kwa hiyo," nikasema, "kama ningeweza kuvuka kilele cha kilma hiki bila wao kuniona, nipande juu kupitia kwenye mreteni huu pale," nikasema, "kama nikizunguka upande huu, kuna mkondo wa kulungu unaoshukia upande huu, ninaweza kukimbia kule na kutoweka njiani. Kisha nitundike kipande kidogo cha karatasi hapa ambapo ninajua nitaendea kidole gani, kwenye genge hili, na kumpata Ndugu Fred kule kwa wakati mzuri."

27 Nilitupa chini mbegu hii ya kishomanguo, nikasahau jambo Hilo. Ndipo nikaanza kutelemka kuvuka kilima kwa urahisi sana kisha nikaangalia nyuma, hawakuniona, basi nikateremka mbio nikafikia kwenye mkondo huu wa kulungu. Nilikuwa nimevaa kofia kubwa pana nyeusi. Nikaanza kukimbia mbio sana kupitia kwenye magenge haya, ndipo likatukia.

Ardhi nzima ilitetemeka, kila mahali. Miamba ukubwa *huo* ikafingirika chini, mavumbi yakiruka namna *hiyo*. Nami nikaangalia, na mbele yangu walisimama Malaika saba; jinsi hasa ilivyokuwa. Nilijisikia kama nilikuwa nimesimama juu mbali sana kutoka ardhini. Kwanza, nilifikiri mtu alikuwa amenipiga risasi, wajua, nikiwa nimevaa hiyo kofia nyeusi; nilionekana kama ngiri, hata hivyo, unajua wao ni weusi. Nilidhani mtu fulani alikuwa amenipiga risasi, karibu … karibu sana. Nami ni—nikaona basi ilikuwa ni nini. Vema, mara tu … Nikapata agizo langu, na Maandiko, "Mihuri Saba ambayo ni zile siri saba." Mnaona?

28 Mtu fulani aliniambia, kasema, "Sasa …" Loo, akasema, "Vema, sasa, siku moja Bwana labda (wewe kwa kuona maono, Ndugu Branham) atakufunulia mambo haya ni nini, sote tunaweza kuwa karibu na

Mungu na tuwe na nguvu zaidi kuliko tunavyopata katika kunena kwa lugha na kadhalika."

Nikasema, "Haiwezi kuwa hivyo."

Maana, mnaona, ninaamini Neno kuwa ni Kweli. Na Biblia ilisema, "Ye yote atakayeongeza neno moja ama kuondoa Neno moja Kwake." Haina budi kuwa katika Neno hili. Mnaona? Ni zile siri ambazo watu hawakuziona. Vema, papo hapo ndipo palitokea Ujumbe wangu wa *Uzao wa Nyoka* na Imani ya kweli ya usalama wa mwamini.

29 Mimi siwadharau ndugu zangu wa Kipresbiteri hapo, na ndugu fulani wa Kibatisti jinsi mlivyo na usalama. Sisemi jambo hili kusudi niwe tofauti, lakini hamkulipata jambo hilo sawa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Lakini, nilikuwa nimekosea, pia. Lakini wakati Malaika anaposimama kutoka Mbinguni na kukwambia, na hili hapa moja kwa moja katika Maandiko, Hiyo ni kweli. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona, Yeye daima hunena sawasawa na Maandiko.

30 Ndani humo niliangalia mpaka hiyo duara ikapaa juu, ikaanza kwenda juu, nao wakabadilika kuwa nuru ya kisiri, kama ukungu. Vivyo hivyo hasa … Ni wangapi waliona picha Yake iliyopigwa huko Houston? Karibu wote. Mnaona? Vema, Hivyo ndivyo hasa hii ilivyokuwa. Iligeuka ikawa jambo lile lile, ilizidi kwenda juu zaidi na zaidi.

Nilikuwa nikikimbia na kukimbia, nikijaribu kumpata Ndugu Fred na hao wengine. Baada ya kitambo kidogo, kama nusu saa baadaye, niliweza kumwona huko chini kabisa, akipunga mikono yake; na Ndugu Gene akija, akipunga mikono. Walijua jambo fulani lilikuwa limetukia. Na kwa hiyo basi nikawafikia. Huyo ni Ndugu Fred anayeketi papo *hapo*.

31 Wakati ilipokuwa ikienda juu, sikujua ya kwamba vituo vya uchunguzi na kadhalika, mpaka kufikia Mexico, vilikuwa vikipiga picha hiyo. Gazeti la *Life* lilichapisha picha Yake lilipokuwa likipaa juu. Na wengi wenu … Hili hapa gazeti la *Life* limechapisha picha Yake. Kitu kisichofahamika hapa, nao walisema hawajui kilikotoka; kiko juu sana. Kiko juu ya maeneo yote ya anga na cho chote kile… Kiko juu sana hakiwezi kuwa ni ukungu, kwa sababu kitu hicho kiko maili thelathini kwenda juu na maili ishiri na saba kutoka upande mmoja mpaka mwingine baada ya kwenda juu kiasi hicho. Hakuna hata unyevu wala cho chote kule, mnaona.

32 Nao waliwazia kuhusu ndege; kwa hiyo wakachunguza mahali pote, hakuna ndege zilizoruka juu siku hiyo. Mnaona, imewalazimu kuchunguza, kwa sababu ya kutikiswa kwa madirisha na kadhalika. "Hakuna ndege juu." Hili hapa moja kwa moja gazetini, litakwambia jambo lile lile. Na—na ikaendelea na kuendelea. Na leo hii moja kwa moja katika …

Hili hapa katika gazeti la Science, ambapo, hawawezi kufahamu. Hawajui ni kitu gani.

Huko Tucson, chuo kikuu, rafiki yangu mmoja alienda kule hivi majuzi naye alikuwa akizungumza nao kuhusu ya jambo hilo. Kasema, "Hatuwezi kuelewa ni kitu gani…"

Nikasema, "Usiseme lo lote, halitafaa kitu. 'Msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe.'" Mnaona? Ni kwa ajili ya Kanisa, kwa Wateule, walioitwa watoke. Mnaona?

33 Na halafu kila mmoja alikuwa anakuja, akisema, "Ndugu Branham, ninaona picha yako hapa. Ninaona *hii*. Mimi …" Unajua jinsi ilivyo. Lakini huo—huo mtandao mrefu kama huu alio nao ndugu huyu hapa ambapo … Samahani. [Ndugu Branham anachukua hiyo picha—Mh.] Hivi ndivyo lilivyoanza kupaa juu, likielekea juu. Kwa kweli *hili* lilikuwa kwenye mkono wa kulia. Nanyi nyote mnakumbuka nilisema, "Yule Malaika maarufu alikuwa ndiye aliyenena na mimi, alikuwa mkono wa kulia," hata kabla halijatukia. Mnakumbuka? Mbawa Zake zilielekea nyuma namna *hiyo*. Hayo ndiyo mabawa hasa ya Malaika huyo wakati alipopaa juu. Mnaona, wakati … Kwa hiyo wakaanza kupiga picha kwa sababu lilikuwa ni la kisiri sana. Lakini wakati picha ya mwisho, wakati ilipojiumba Yenyewe ndani ya mbingu na kadhalika, ndio hii hapa kama vile *Look* hapa lililivyoichukua. Mnaona jinsi lilivyopaa juu mara tu walipoanza kuliona, mnaona. Ndipo hapo ikaja ninii—ile picha yenyewe halisi na ya mwisho, wakati lilipoumbika.

34 Hawajui mahali lilipotoka au mahali lilipoenda, wangali hawajui. Sayansi imeduwazwa kabisa juu yake, haijui kile kilichotukia. Lakini tunajua; "Kutakuwa na ishara mbinguni juu." Tunajua jambo hilo. Mnaona? Naye aliahidi mambo haya. Mnaona? Na sababu tu ya hii kuruhusiwa kupigwa…

Lakini ninajua sisi ni watu tu wa nyumbani hapa asubuhi ya leo. Kama niliwahi kujifanya mjuaji kwenu ndugu ama kwenu dada, naomba mnisamehe. Simaanishi kuwa hivyo. Ninasimama…nimeketi hapa asubuhi ya leo nikizungumza mbele ya watu ambao ni wasomi, watu wenye bongo; mimi si— sina elimu, hata siwezi kutamka Maandiko yangu vizuri. Nina mlango mmoja wa kusoma asubuhi ya leo, mimi… nilikuwa nimwombe mmoja wa ndugu hapa anisomee mlango huo, maana hata siwezi kutamka majina yaliyo katika mlango huo, I Mambo ya Nyakati 13, (kama ukipenda, Ndugu Jack, unaweza kuutafuta), kwa ajili ya somo langu. Hata si—siwezi kutamka majina hayo, nitamwachia asome, maana yeye anaweza kuyatamka.

Nami ninajua ninazungumza na watu werevu. Lakini, ndugu, mambo haya yanafanyika kusudi msiangalie kutokujua kusoma kwangu, bali mwamini ninawaambia Kweli. Ni Mungu akiwaambia Kweli. Hiyo ni Kweli. Mnaona?

35 Sasa, na wakati ninapozungumza juu ya madhehebu, sikusudii mwe wakatili sana na… La, simaanishi msiende kanisani kwenu. Nendeni kanisani kwenu, yale unayopaswa kufanya. Bali msijiunge na hayo madhehebu, kwa sababu siku moja nitawaambia na kuwathibitishia kwa Maandiko, ni alama ya mnyama. Nanyi kumbukeni tu, ni alama.

36 Ninahubiri … Singehubiri jambo hilo kwenye kanisa la Ndugu Jack, yeye angeniambia, "Endelea na kuhubiri"; lakini ninaenda Maskanini, utachukua kama masaa manne. Na somo langu ni, "Yule mnyama hapo mwanzo na yule mnyama mwishoni, kwa njia ya nyoka." Mnaona? Inachukua kama masaa manne. Nimeandika Maandiko yangu yote. Yule mnyama tangu mwanzo, yeye alikuwa ni yule mnyama kwenye bustani ya Edeni, yeye ndiye yule mnyama mwishoni, na anaonyesha ya kwamba yeye ni mtu wa kidini na dhehebu (lililounda madhehebu); na kuja moja kwa moja kwenye mkondo wake, na kuwathibitishia kwa Maandiko kwamba ndivyo ilivyo. Sikujua jambo hilo mpaka Roho Mtakatifu aliponipa hilo hivi majuzi kule.

37 Sasa, katika jambo hili, nilikuwa nikiangalia jambo hili siku moja, nikisimama, na kitu fulani kikaniambia … nikiiangalia, nami nikawazia … Ndugu Hickerson, mmoja wa wadhamini wangu … ama mashemasi katika kanisa huko Jeffersonville … Kama siamini kwenda kanisani, kwa nini nina kanisa? Tulikuwa nayo kila mahali nchini, yameunganishwa hivi majuzi usiku, kila maili mia mbili mraba kulikuwapo na kanisa langu.

Sasa, hii—picha hii, nilikuwa nimesimama, nikiiangalia, na kitu fulani … Nilikuwa nimesimama chumbani mwangu. Kitu fulani kilisema, "Igeuze upande wa kulia." Nilisikiliza.

Ninajua hilo linasikika kama mtu fulani ambaye amerukwa na akili kidogo, lakini, mnaona, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, mambo haya yote makuu ni ya kisomi sana … Sasa, mimi sipingi jambo hilo. Kumbukeni, hatuna budi kuwa pelekeni watoto wenu shuleni wapate elimu na kadhalika, lakini nitawaambia papa hapa sasa hivi, haitawasaidia hata kidogo katika ulimwengu ujao, kwa maana kutakuwako na ustaarabu mwingine, yote haya mbali sana na huu. Ustaarabu huo hata hautakuwa na … Hautakuwa na shule zozote ndani yake, hautakuwa na mauti yoyote ndani yake, hautakuwa na dhambi yo yote ndani yake. Huu una yote hayo; haidhuru tuna ustaarabu kiasi gani,kifo kinazidi kuongezeka wakati wote. Mnaona? Huo hautakuwa na kifo. Lakini sasa inatubidi kuwa na shule, inatubidi kuvaa nguo, sisi …

38 Nilikuwa nizungumze asubuhi ya leo juu ya *Edeni ya Shetani* (wengi wenu mna kanda yake), *Edeni ya Shetani.* Yeye ameunda bustani nyingine ya Edeni, na imechukua miaka elfu sita kuifanya, kama tu vile Mungu alivyofanya Yake hapo mwanzo. Mungu aliifanya Edeni Yake, na Shetani akaiharibu. Sasa Shetani ameifanya Edeni yake mwenyewe, na Mungu ataiangamiza (hiyo ni kweli) na kuweka Yake Mwenyewe.

Kitu fulani kikaniambia, "Igeuze mkono wa kuume."

Nikawaza, "Nafikiri ninaiangalia vizuri."

Kasema, "Igeuze *kulia*." Mnaona?

Nikawazia, "Labda sauti hiyo inamaanisha niigeuze kwenye upande wa kuume." Na nilipofanya hivyo, mnaona ni kitu gani: *Kichwa cha Kristo* cha Hofmann, akiwa na umri wa miaka thelathini na mitatu. Hapa, angalia hapa ndani, angalia ndevu Zake nyeusi, uso Wake, macho Yake, pua Yake, na cho chote kile. Angalia sehemu katika nywele Zake hapa ikichipuka. Naye amevaa wigi na hiyo wigi nyeupe ya Malaika kuonyesha ya kwamba Ujumbe wa kwamba Yeye ni Mungu ni Kweli. Yeye ndiye Hakimu Mkuu wa ulimwengu, Hakimu Mkuu wa Mbingu na nchi. Yeye ni Mungu, wala si kitu kingine ila Mungu. Yeye ni Mungu aliyedhihirishwa katika umbo la kibinadamu linaloitwa Mwana wa Mungu, ambapo Mwana alikuwa ni kinyago. Na kama hilo halifanyi Ujumbe wetu kuwa sahihi kabisa: kutambulishwa kwa Maandiko, kutambulishwa katika huduma, kutambulishwa na Uwepo Wake, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa hiyo hiyo Mihuri Saba ni Kweli, ndugu. Huenda msikubaliane nayo, lakini ketini chini tu na msome kwa moyo mkunjufu wakati mmoja, acheni tu Roho Mtakatifu awaongoze kutoka…

39 Hapa, wakati Ndugu Jack … Nilimwita kabla ya kuhubiri jambo hili na kuzungumza naye wakati mmoja kuhusu "Hii wigi nyeupe ilikuwa ni nini?"

Akasema, "Vema, Ndugu Branham, ninatangaza ya kwamba ilikuwa katika…ilikuwa ni baada ya kufufuka Kwake katika mwili Wake uliotukuzwa." Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Jack. Na kuna … Sijui juu ya mtu ye yote ulimwenguni ninayeweza kutegemea mafundisho yao juu ya theolojia na kadhalika zaidi kuliko ninavyotaka kumtegemea Ndugu Jack Moore na Ndugu Vayle, na mtu kama—kama hao, wanatheolojia halisi walisoma vitabu vya kila namna na mitazamo mbalimbali kutoka kila kitu. Vema, lakini, mnaona, hata na jambo hilo, na rafiki wangu msiri, ni—ni—nisingeweza kulipokea, kulikuwako na kitu fulani ambacho hakingeweza kulipokea.

40 Na halafu wakati linapokuja, hili, ndipo ninaona ni kitu gani. Hizi hapa ndevu Zake nyeusi. Mnaliona, nadhani. Mnaona? Ndevu zake nyeusi na nywele nyeusi, macho Yake, pua, kila kitu, kikamilifu kabisa, na hata sehemu katika nywele Zake ikija upande huu. Yeye ni Mungu! Mnaona? Naye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na hili ni gazeti la *Look* … ama gazeti la *Life*. Nafikiri hili ndilo … Ninasahau ni suala gani sasa; loo, tarehe kumi na saba, 1963. Hapo ndipo linapotokea, kama mtu yeyote anataka gazeti. Ni picha ile ile iliyo na Rockereller na na nanii wake—mke wake upande wake wa nyuma. Na hili ndilo gazeti jipya la *Sayansi* ambalo "bado ni siri."

41 Ni kwa nini nilisema mambo haya? Ili yawape mwelekeo mdogo wa mambo tunayojaribu kusema, ambayo Mungu anayatambulisha mbinguni na nchini kwamba ni kweli, huu utambuzi, maono. Tuna uigaji mwingi, sisi daima. Lakini kumbukeni, kabla hapajakuwepo na dola ya bandia, hapana budi kuweko na dola ya kweli; kwanza hapana budi kuweko na dolla ya kweli, halafu zinatolewa kutoka kwa hiyo. Kama tu vile tulivyokuwa na Musa halisi na Haruni halisi, basi tulikuwa na Yambre na Yane baada yao. Mnaona jinsi yote yanavyokuja? Wanaliona kisha wanajaribu kuiga hilo, wakati kweli kuna *moja* iliyo ya asili Hiyo ni kweli. Sio kusema hilo kudhuru ama kudhalilisha, ama kuweka kitu fulani vibaya, bali kwa ajili ya Kweli tu; kujua ya kwamba mimi …

42 Ninakuwa mzee, nami najua wakati wangu si mrefu sana. Kama Yesu, akikawia, naweza … ningeweza kukaa muda kidogo; bali ninajua ya kwamba siku moja moyo huu utafanya mapigo yake ya mwisho, nami ninaingia kwenye chumba kikubwa, cheusi pale kinachoitwa mauti. Lakini wakati jambo hilo linapokuja, sitaki kitu chochote cha kunilazimu kuangalia nyuma, kujaribu kutubu. Ninataka, nitakapofikia wakati huo, niwe msafi na msafi kwa neema ya Mungu. Ninataka kujifunika mavazi ya haki Yake, ninapoingia mle, nikiwa na jambo hili moja moyoni mwangu: ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake; na wakati atakapoita, nitatoka miongoni mwa wafu na kuishi pamoja Naye milele. Na ni kusudi langu hapa sasa kujaribu kumfanya kila mtu … si kubadilisha theolojia zenu ama cho chote kile, bali kuongeza imani yenu katika ahadi ya Mungu ya siku hii.

Sasa hebu tuombe:

43 Mungu mpendwa, sisi ni watu wenye shukrani asubuhi ya leo, lakini hata hivyo, Bwana, tunaishi katika ulimwengu wenye giza ambao … Hakuna hata mmoja wetu hapa asubuhi ya leo, Baba, ila yule anayejisikia ya kwamba tu—tunataka kutembea karibu zaidi na Wewe, tunataka huo—huo mguso Wako maishani mwetu ambao unaweza kututia moyo na kutufanya tupate kubadilika ili kwamba Wewe unaweza kutubadilisha wakati wowote, kutufinyanga kuwa wana na binti za Mungu. Hilo—hilo ndilo kusudi letu hapa, Baba, hilo—hilo ndilo kusudi langu pekee nililo nalo ni kujaribu ku—kuishi mbele Zako na kulipata Neno Lako na kulirudia kwa wanaume na wanawake ambao … si kuwa mtu tofauti bali kujaribu kumheshimu Yeye aliyenipa Uzima. Jalia hilo, Bwana.

44 Jalia kusiwe na mtu hapa leo … Ama—ama kama … Tumeunganishwa asubuhi ya leo, kote nchini, tena. Jalia asiwepo mtu aliye kwenye eneo la sauti yetu atakayelazimika kuingia katika kile chumba kikuu bila kukujua Wewe katika nguvu za kufufuka Kwako. Kama kuna wenye dhambi mahali fulani kote nchini, ambao … ama katika jengo hili, ukumbi huu mkuu, wanaoketi hapa asubuhi ya leo. Kama kuna wale wasiokujua Wewe, jalia hii iwe ndiyo siku ambayo dhamira zao zitatikiswa, zitaamshwa, nao watatambua ya kwamba hawajui ni dakika gani ambayo tunaweza kuitwa ama tuitwe tukujibu kwa ajili ya maisha yetu, huko Juu. Na kama jina letu lingali liko kwenye kitabu hicho cha ubua, tutaangamia; lakini kama liko kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ule Uhai halisi, basi tumeokoka.

Na jalia, Bwana, wakati Uhai huo ukisafiri kutoka katika jani na kuingia kwenye chavua, hadi kwenye kapi, halafu kwenye chembe, wakati wakipita asubuhi ya leo kama kuna Uhai fulani unaoingia kwenye chembe iliyo kule nyuma katika huo ubua, utoe leo, Bwana, naomba huo ufuate kusogea kwa ile chembe, kwa kuwa tunaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

45 Samahani kuchukua muda mwingi sana. Nilisahau hata kwamba haya yalikuwa yako kwenye kipindi cha kule nje, kipindi cha simu.

Sasa hebu na tufungue kwa ajili ya kusoma kwetu. Na Ndugu Jack, una Biblia yako pale? Ninapopata Maandiko yangu, nitamwomba Ndugu Jack asome Maandiko haya kwa sababu siwezi kutamka majina haya. Vema. Iko katika Mambo ya Nyakati ya Kwanza 13. [Ndugu Jack Moore anasema, "Sura nzima?" —Mh.] A-ha.

[Ndugu Jack Moore asoma Mambo ya Nyakati ya Kwanza 13:1-14:

> *Kisha Daudi akafanya shauri na maakida wa maelfu, na maakida wa mamia, naam, na kila kiongozi.*
>
> *Daudi akawaambia jamii yote ya Israeli, Likiwa jema kwenu, tena likiwa limetoka kwa Bwana, Mungu wetu, na tutume watu huku na huku mahali pote kwa ndugu zetu waliosalia katika nchi yote ya Israeli, ambao pamoja nao makuhani na Walawi wamo ndani ya miji yao*

*yenye viunga, ili wakusanyike kwetu;*

*Nasi tujirudishie tena sanduku la Mungu wetu; maana hamkuuliza neno kwa hilo katika siku za Sauli.*

*Nao jamii nzima wakasema ya kwamba watafanya hivyo; kwa kuwa neno hilo lilikuwa jema machoni pa watu wote.*

*Basi Daudi akawakusanya Israeli wote, toka Shihori, kijito cha Misri, hata pa kuingilia Hamathi, ili kwamba walilete sanduku la Mungu kutoka Kiriath-yearimu.*

*Basi Daudi akapanda, yeye na Israeli wote, mpaka Baala, ndio Kiriath-yearimu, ulio wa Yuda, ili kulileta toka huko sanduku la Mungu, Bwana akaaye juu ya makerubi, lililoitwa kwa Jina lake.*

*Wakalipandisha sanduku la Mungu juu ya gari jipya kutoka nyumba ya Abinadabu; na Uza na Ahio wakaliendesha lile gari.*

*Wakacheza Daudi na Israeli wote, mbele za Mungu, kwa nguvu zao zote; na kwa nyimbo na kwa vinubi, na kwa vinanda, na kwa matari, na kwa matoazi, na kwa tarumbeta.*

*Hata walipofika penye uga wa Nakoni, Uza akaunyosha mkono wake alishike sanduku; kwa maana wale ng'ombe walikunguwaa.*

*Ndipo hasira ya Bwana ikawaka juu ya Uza, naye akampiga, kwa sababu alilinyoshea sanduku mkono wake, hata akafa pale pale mbele za Mungu.*

*Naye Daudi akaona uchungu, kwa kuwa Bwana amemfurikia Uza; akapaita mahali pale Peres-uza hata leo.*

*Naye Daudi akamwogopa Mungu siku ile, akasema, Nitajileteaje sanduku la Mungu kwangu?*

*Basi Daudi hakujichukulia sanduku mjini mwa Daudi, ila akalihamisha kando na kulitia nyumbani kwa Obed-edomu Mgiti.*

*Sanduku la Mungu likakaa na jamaa ya Obed— Obed-edomu, nyumbani mwake, muda wa miezi mitatu; naye Bwana akaibariki nyumba ya Obed-edomu, na yote aliyokuwa nayo.*

46 Asante, Ndugu Moore, kwa kunisomea Maandiko. Sasa, samahani nisingeweza kusoma hayo mimi mwenyewe, bali si—singeweza kufanya hivyo.

Sasa nataka mfungue pamoja nami kwenye Marko 7:7, nasi tutasoma vifungu saba vya kwanza vya Marko Mtakatifu sura ya 7.

*Kisha Mafarisayo, na baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu, wakakusanyika mbele yake,*

*Wakaona wengine katika wanafunzi wake wakila vyakula kwa mikono najisi, yaani, isiyonawiwa.*

*Kwa maana Mafarisayo na Wayahudi wote wasiponawa mikono mpaka kiwiko, hawali, wakishika mapokeo ya wazee wao.*

*Tena wakija kutoka sokoni, hawakutawadha, hawali. Na yako mambo mengine yalikuwa—yalikuwa…waliyopokea kuninii…kuyashika,… kuosha vikombe, na midumu, na vyombo vya shaba, na vya mezani.*

*Basi wale Mafarisayo na waandishi wakamwuliza, Mbona wanafunzi wako hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee, bali hula chakula kwa mkono najisi?*

*Akajibu akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa midomo ila mioyo yao iko mbali nami.*

*Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*

Hebu na tuombe.

47 Mungu mpendwa, litukuze Neno Lako sasa, na jalia litimize yale yaliyokusudiwa. Tutumie kama vyombo kulinena, na masikio yetu kusikia kutoka Kwako, na mioyo yetu kulipokea. Tunaomba katika Jina la Yesu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

48 Sasa, somo langu kwa muda mfupi ni hili … Mimi …

Tuko kwenye muunganiko wa simu kitaifa asubuhi hii. Nami nasikia ya kwamba rafiki yangu mzuri, Roy Borders, anasikiliza, amehangaika sana kuhusu jana usiku. Ningesahau ya kwamba tulikuwa kwenye redio … ama mawasiliano haya jana usiku. Roy, popote ulipo, kama uko kule San Jose kanisani, ama ama kwenye kanisa la Ndugu McHughes, ama po pote ulipo, usiogope, ndugu yangu, kila kitu kitakuwa sawa. Tulieni, ninyi tu … Yeye atanijulisha, Roy; usijali, mwanangu, uwe na imani katika Mungu.

49 Somo langu asubuhi ya leo ni: *Kujaribu Kumtumikia Mungu Bila ya Kuwa Ni Mapenzi ya Mungu.* Sasa, hilo ni fungu la ajabu, nami ninatumaini ya kwamba Bwana atatufunulia jambo hili sasa. Kumbuka, "Kujaribu kumtumikia Mungu bila ya kuwa ni mapenzi ya Mungu." Sasa, hilo linaonekana ni la ajabu sana. Lakini, katika jambo hili, labda Mungu anaweza kutusaidia.

50 Jambo lingine ningependa kusema asubuhi ya leo, ya kwamba tuna furaha kuwa na miongoni mwetu rafiki yangu, rafiki mpendwa sana, jamaa mdogo. Wengi wenu ninyi watu kwenye redio sasa mnaweza … ama ninii … kwenye mawasiliano ya simu, mnajua huyu ni nani. Leo ni siku yake ya kuzaliwa, mwenye umri wa miaka tisini na mitatu, Ndugu Bill Dauch anayeketi hapa mbele yangu, mwenye umri wa miaka tisini na mitatu.

Miaka kadhaa iliyopita daktari alisema, "Hawezi kuishi." Nimemwona tu ameketi hapa sasa. Chini ya hema ya oksijeni, na mke wake wa kupendeza alinipigia simu na kusema, "Ndugu Branham, kama unatarajia kumwona rafiki yako wa zamani, Bill, akiwa hai, afadhali uje mara moja."

51 Nami … Moja ya tairi zangu ilikuwa imekatwa upande mmoja, gurudumu langu lilikuwa limepasuka, nami nikararua tairi la gari langu nikijitahidi kwenda kumwahi. Nilikuwa ndiyo kwanza ninakuja kutoka kwenye ki—ki— kituo, kituo cha petroli, na ninatoka msalani ambapo nilikuwa nimesimama huko Ohio nikikazana kumwahi, na nilipokuwa nikitoka nikaona ono. Na hapo alisimama Ndugu Dauch, amesimama kanisani huku ametoa mkono wake; likabadilika, ndipo nikakuona ukishuka kuja barabarani na kunipa mkono. Kasema, "Nenda kamwambie, 'BWANA ASEMA HIVI.'"

Alikuwa na umri wa kama miaka tisini wakati huo. Alikuwa na mshtuko wa moyo pamoja na moyo kuziba, na kusita kabisa kwa moyo. Daktari hodari sana. Mtu huyo si … hataki … La, sitasema jambo hilo. Yeye ni mtu tu anayeweza kumudu … kupata daktari yeyote ambaye angetaka. Alikuwa na daktari mzuri sana wa Kiyahudi aliyekutana nami ukumbini na kusema, "Hakuna nafasi kwake kuishi."

Basi nikaingia ndani na kupenyeza mkono wangu chini ya kile kihema cha oksijeni, nikasema, "Bill, unaweza kunisikia?" Alitikisa kichwa chake. Nikasema, "BWANA ASEMA HIVI, 'Hutakufa sasa.'"

52 Juma moja tangu wakati huo, nilipofika mimbarani kuhubiri Ujumbe wangu, huyu hapa Ndugu Dauch anakuja akitembea jengoni. Na nilipoenda kwenye Mkahawa wa Furr, upande wa pili…ninamaanisha Blue Boar, kwenda huko Louisville, huyu hapa akitoka kwenye gari, akishuka barabarani, ametoa mkono wake; sawasawa na Neno la Bwana. Na hiyo ni miaka mitatu ama minne iliyopita; na huyu hapa ameketi huko chini kabisa, huko Shreveport (anavuka nchi, si kwa ndege sasa, kwa gari) a-ha, ameketi hapa asubuhi ya leo. "Heri ya siku ya kuzaliwa, Ndugu Dauch." Hiyo ni kutoka kila mahali nchini, kutoka kila mahali. "Mungu akubariki!"

53 Nilimbatiza, baada ya kuwa wa utatu, nilimbatiza wakati aliponinii…ilikuwa mmoja wa mikutano yangu ya kwanza, wakati ilipombidi Ndugu Banks Wood kumpatia nguo zake (yeye ni mtu mkubwa, kama mnavyoona), ndipo akaingia katika kidimbwi nami nikambatiza akiwa na kama miaka themanini na mitano ama tisini, katika Jina la Bwana Yesu. Yeye alisema kamwe asingejisikia vizuri mpaka alipopata usalama huo wa kitu fulani. Ndipo akapokea siku ya kuzaliwa ambapo hatazeeka kamwe. Hiyo ni kweli, ile Nchi kuu. Yeye hata anatarajia kuishi apate kuona Kuja kwa Bwana; inawezekana. Lakini kama angelala, yeye … nasi tuko macho wakati huo, atakuja kwanza. Sawa. Kwa hiyo, Ndugu Dauch, hakuna njia sasa ya kukosa jambo hilo. Wewe uko kwenye njia sahihi. Kaa pale, ndugu yangu, na Mungu akubariki. Nami ninamshukuru Bwana kwa mtu mzuri kama huyo, na kwa kumpa miaka hii yote.

54 Katika Kitabu cha Mambo ya Nyakati, "Kujaribu kumtumikia Mungu bila ya mapenzi Yake." Mungu ni mwenyezi, kwanza, tunataka tulielewe. Watu siku hizi wanashangaa ni kwa nini hatuwezi kuwa na ufufuo. Je! unaamini Mungu ni mwenyezi? Mnaona, Biblia inanena hivi.

Nasi tunajaribu … Kama nilivyokuwa nikijadiliana na kundi la ndugu zangu wazuri, ndugu wa Kibatisti, si muda mrefu uliopita, nao wakasema, "Ndugu Branham, tunaweza tu kuwa na uamsho tunapochukua Neno, neno kwa neno, ukurasa kwa ukurasa, herufi kwa herufi."

Nami nikasema, "Ninaamini pia, ukurasa kwa ukurasa." Yeye alisema … Nikasema, "Wamekuwa wakijaribu kufanya jambo hilo wakati wote."

Yeye alisema, "Lakini hatuna budi kupata tafsiri ya Kiyunani ya Neno, kile Kiyunani inachosema."

Nikasema, "Sijasoma mengi sana, bali nikisoma historia ya kanisa, na Baraza la Nikea, na Baraza la kabla ya Nikea, na akina baba wa Nikea, na kadhalika, walikuwa wakibishana huko nyuma kuhusu

Kiyunani. Hiyo ni miaka elfu mbili iliyopita. Mmoja alisema, 'Inamaanisha *hivi*,' na mmoja anasema, 'Inamaanisha *vile*. Neno la Kiyunani linamaanisha *hivi*.'"

55 Ni kama tu lugha yetu; neno kuona. Ukitumia neno see, unaweza kumaanisha "eneo la maji, nasikia," ama mambo mengi. *Bored* (chimba), "kuchimba shimo, kutengeneza barabara," ama—au "you bored me (ulinichosha)," ama "you paid my board (ulinilipia malazi)," ama lingeweza kumaanisha cho … mambo mengi. Na voweli hizo ndogo, na kadhalika, zinabadilisha maana yote. Kwa hiyo kamwe hutalifanya namna hiyo. Mungu aliliandika namna hiyo, kwa sababu …

Na Neno lote limevuviwa, Naye alisema ya kwamba, "Nakushukuru, Baba, ya kwamba umewaficha mambo haya kutoka kwenye macho ya wenye hekima na akili ukawafunulia" (amina) "watoto wachanga wanaoweza kujifunza." Ni ufunuo Wake, kama nilivyosema jana jioni, "Atawafunulia watoto wachanga."

Nikasema, "Haitafanikiwa, bwana." Nikasema, "Ufufuo hautakuja kamwe mpaka Mungu, mwenyezi Mungu, autume; ndipo basi anaweza kumchukua maskini mjinga fulani ambaye hata hawezi kuandika jina lake, na kutenda kazi pamoja naye, ambaye hata hajui Kiingereza kizuri sembuse Kiyunani."

56 Hivyo ndivyo alivyofanya katika wakati Petro alipohubiri kwenye Pentekoste, mwajua, hata asingeweza kuandika jina lake, asiye na maarifa na asiye na elimu. Lakini Mungu hufanya mambo kwa njia ya ajabu sana kwa kuwaza kwetu kiakili. Hilo linamfanya Mungu. Kama angalichukua kundi la wanatheolojia na watu mashuhuri, na kadhalika, wangesema, "Yule Kayafa mwenye bongo, mnaona, alilipata vizuri kabisa." Lakini Mungu alishuka akaenda na kuwachukua wavuvi ambao hata hawangeweza kuandika jina lao, na hao ndio aliowachukua. Huyo ni Mungu, huchukua kitu ambacho si kitu na kufanya kitu kutokana na hicho kwa utukufu Wake Mwenyewe. Alichukua machafuko na akafanya Edeni. A-ha, ni Mungu.

57 Sasa, kama kuna mtu yeyote aliye na mitambo ya uamsho, ni ndugu yetu mtukufu, Billy Graham. Lakini mitambo ni sawa, lakini mitambo haitauendesha, inahitaji nguvu za kuendesha upate kwenda. Unaweza kuunda motokaa, uweke viti vizuri ndani yake, pistoni nzuri na—na uthibitishe kwa sayansi vile unavyoweza kufanya; lakini isipokuwa nguvu za kuendeshea ziwemo, hilo ni bidhaa iliyokufa tu.

Kwa hiyo, katika uamsho wa Wesley, mmoja wa ufufuo wetu uliopita kabla ya ufufuo wetu wa Kipentekoste, hakuna aliyejua kilichouanzisha ufufuo huo, ni kundi tu la watu.

Sasa, tutakapopata yote…rafiki yetu, Billy Graham, atawakusanya Wapresbiteri wote, na Waluteri, na Wapentekoste, na kila kitu pamoja, aende mjini na huko watakuwa na kusanyiko kubwa la maelfu, na elfu thelathini watakuja (katika majuma mawili) na kumpa Kristo moyo wao; unarudi majuma mengine mawili wala huna hata mmoja. Mnaona, hiyo ndiyo mitambo. Lakini hebu Mungu katika neema Yake kuu anene tu na maskini mjinga fulani, tuseme, mtu ovyo; aruhusu Roho Wake ashuke mjini wala hakuna mtu anayeweza kufanya kazi, wanawake hawawezi kuosha vyombo, mjakazi hawezi kutengeneza kitanda, wanapiga makelele na kulia huku mikono yao iko juu hewani. Huo ni uamsho, huo ni katika mapenzi ya Mungu.

58 Ilisemekana ya kwamba baadhi ya watu mashuhuri kutoka kanisani walienda huko Wales kufahamu, ama kujua mitambo yote ilikuwa ni nini katika ule ufufuo, wakati wa uamsho wa Kiwelshi. Na wakati walipotoka kwenye meli na makofia yao marefu, na kosi zao zimepinduliwa; wakamwona maskini polisi mmoja akishuka barabarani, akizungusha-zungusha fimbo yake namna hiyo, anapiga mbinja; wakasema, "Muungwana, je! unaweza kuniambia mahali ufufuo wa Kiwelshi ulipo?"

Akasema, "Naam, ndugu zangu, mnasimama katikati yake!" A-ha, a-ha, a-ha. Akasema, "Mnafahamu, mimi ni uamsho wa Kiwelshi," kasema, "kwa sababu uamsho wa Kiwelshi umo ndani yangu."

59 Huo ni uweza! Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya, na Yeye pekee ndiye mwenye haki ya kutuma uamsho. Si kuunganisha mitambo, ni kuomba Mungu atume nguvu—nguvu za kuendeshea.

Yeye hufunua tu Neno Lake katika waliochaguliwa tangu zamani. Sasa, ninapotumia neno *kuchagua tangu asili* … Sasa, ni neno baya kutumia hadharani, hasa tunapokuwa na umati wa watu waliochanganyikana kati ya Waarmini na Wakalvini. Wala si … Nimewaomba msifikiri ninajua yote, lakini wote wawili wamekosea kulingana na Maandiko. Neema ni yale Mungu aliyonitendea, matendo ndiyo ninayomfanyia. Mnaona? Hapo ndipo umelipata. Kama ukipanda moja ya matawi hayo, hakika utajikuta kwenye ncha ya hilo tawi wala huwezi kurudi. Kitabu cha Waefeso kinaunganisha hayo pamoja, nafikiri.

Sasa, lakini neno, ninapolitumia, kuchaguliwa tangu asili, sidhani ya kwamba mimi ni … hilo ndilo neno pekee ninalojua jinsi ya—kufanya … Ni kujua tangu zamani kwa Mungu, mnaona, kwamba Yeye alijua. Yeye—Yeye hawezi kusema … Yeye—Yeye alikufa ili kwamba watu wote wapate kuokolewa, alifanya hivyo, bali kwa kujua Kwake tangu asili alijua ni nani angeokoka na ni nani asingeweza. Mnaona? Hicho ndicho anachojua, mimi sijui na ninyi hamjui, kwa hiyo tunatumia wokovu wetu wenyewe kwa hofu na kutetemeka.

60 Sasa, lakini Mungu ameweka Neno Lake, na ameweka katika nyakati zote. Kujua Kwake tangu zamani kumemfanya aweke kanisani, na katika watu, mambo fulani ambayo alifanya tangu mwanzo. Na halafu Injili inayohubiriwa kwa wakati *huo* inafunuliwa tu kwa watu fulani, hao wengine hawalioni. Mnaona? "Asante, Baba Wewe umeyaficha mambo haya kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na kuyafunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza." Mnaona, huko ni kuchaguliwa tangu asili. Si kwamba alifanya jambo hilo kwa, unasema, "Nitakuchagua wewe, bali wewe sitakuchagua." Kwa kujua Kwake tangu zamani, Yeye alijua yale ungefanya.

Kwa Yeye kutokuwa na kikomo … Unaamini Yeye hana kikomo? Kama sivyo, Yeye hawezi kuwa Mungu. Basi, unawazia, kwa kuwa hana kikomo: Yeye alijua kila kiroboto atakayekuwa duniani, kwamba ni mara ngapi hao viroboto wangepepesa macho yao, ni shahamu kiasi gani yaliyokuwako katika kila kiroboto, kila jani la nyasi ambalo angeketi juu yake; huko ni kutokuwa na kikomo. Nasi tuna kikomo, tunajikwaa gizani. Mungu alitufananisha na kondoo, na hatuna budi kuwa na Kiongozi. Na kiongozi huyo si mwanadamu, huyo Kiongozi ni Roho Mtakatifu, Roho wa Kristo miongoni mwetu. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena." Mwili Wake wa kawaida uliinuliwa hadi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, ambapo Roho *alikuwa* juu ya Kiti cha Enzi; sasa Kristo yuko kwenye Kiti cha Enzi, Yesu. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari, hata ndani yenu." Kiti cha Enzi cha Mungu, cha Kristo, kimewekwa moyoni mwako; Naye ameketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, lakini katika ule Utawala wa Miaka Elfu Yeye ataketi kwenye Kiti Chake Mwenyewe cha Enzi; ambapo, Yeye aliapa ya kwamba angemwinua mtu huyu, Mwanawe, Mwana wa Daudi, aketi kwenye Kiti Chake cha Enzi.

61 Sasa, Yeye hufunua mambo kwa kujua Kwake tangu zamani kwa hao ambao Yeye amewachagua kwa ajili ya mambo haya, la sivyo hawalioni. Simama papo hapo, ukiliangalia moja kwa moja, wala huwezi kuliona.

Ni wangapi waliopata kuona ile picha ya ng'ombe kichakani, ambayo inakubidi tu kuangalia na kuangalia? Je! Ulipata kuona jambo hilo? Ama, umeona picha ya Kristo kichakani, ama angani, ama mawinguni? Mnaona, huyo mchoraji ameweka hilo vizuri sana hata inakubidi kuliangalia kwa njia fulani tu. Vema, basi, wakati unapoiona mara moja, huwezi kuona kitu kingine ila hiyo. Kila wakati ukiangalia, hiyo hapo. Ni wangapi wameona hizo picha? Vema, hakika mmeziona.

Vema, hivyo ndivyo Kristo alivyo, Yeye Mwenyewe, Injili, Ujumbe ulivyo. Wakati unapoona Ujumbe wa wakati huu, hakuna kitu kingine unachoweza kuona ila Hicho. Hivyo tu. Kila kitu kingine kimetoweka, kilichobaki ni kijazio tu, mnaona, mnaona, wakati unapoona Ujumbe mara moja!

62 Hiyo ni—ilikuwa katika wakati wa Nuhu. Wakati Nuhu na kundi lake … angalia jinsi … Walipouona Ujumbe, hakuna kitu kingine kilichokuwa muhimu. Wakati kundi la Musa walipouona, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la Yohana walipouona, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la Yesu walipouona, hawakujali jambo lingine. Wakati kundi la mitume walipoona jambo Hilo, hakukuwa na jambo lingine. Wakati kundi la Luther walipouona, kundi la Wesley walipouona, kundi la Kipentekoste walipouona, hawakujali jambo lingine, waliacha kila kitu. Kwa nini? Kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye alichagua tangu asili mambo haya kutukia.

63 Yeye huchagua mtu Wake Mwenyewe kwa kujua Kwake tangu zamani. Kama vile alivyosema katika Warumi 8 hapa, ya kwamba Esau … ili kwamba—kwamba uteuzi wa Mungu uweze kusimama imara. Kwamba Esau na Yakobo wote wawili walizaliwa na wazazi watakatifu, mapacha, ili kwamba kuteua Kwake kupate kusimama imara na kuwe ni kweli, Yeye alisema, "Ninamchukia Esau, na ninampenda Yakobo," kabla hata mmoja wa hao wavulana kuzaliwa. Mnaona? Yeye anajua kilicho ndani ya mwanadamu, alijua tangu mwanzo ilikuwa ni kitu gani, kwa hiyo Yeye anaweza kufanya kila kitu kitende kazi kwa wakati wake kabisa. Sisi huwa na wasiwasi sana na kuhangaikahangaika; hujapata kumwona Yeye akihangaika, hawahangaiki. Mnaona? Kila kitu kinatenda kazi sawasawa, barabara kabisa, saa inasonga mbele.

Mambo haya yanayopaswa kutukia, wanawake hawa wote wenye nywele fupi, na wanaume hawa wakivaa … kama wana nywele kama za wake zao. Ninawaona, kabisa, wana hizo rola za kutilia mawimbi nywele zao, wanaziweka mawimbi hapa mbele. Ni upotovu ulioje! Hayo ndiyo matokeo ya Edeni ya Shetani. Na mfanye kama yeye: yeye anajaribu kukata nywele zake kama mumewe; mumewe akiachilia nywele zake zikue kama mke wake. Naye mwanamke anavaa nguo za mwanamume, naye mwanamume anavaa nguo za ndani za mwanamke. Mnaona, haya basi. Mwanamke anakuwa kama mwanamume, naye mwanamume anakuwa kama mwanamke. Mnaona, ni Edeni ya Shetani, kinyume na kile Mungu alichokiumba hapo mwanzo. Hiyo ni Kweli.

64 Nisipoanza, kamwe hatutaingilia jambo hili. Lakini mambo haya, na njia ya Yeye kufanya jambo hilo, na ni nani atakayefanya jambo hilo, hiyo ndiyo njia Yake Mwenyewe aliyochagua, Yeye huchagua. Hivyo ndivyo anavyotaka ifanywe.

Kama nilivyomsikia Ndugu Pearry Green, mchungaji wetu huko Tucson, akihubiri hivi majuzi usiku juu

ya jinsi Mungu alivyofanya vitu namna fulani (ninasahau somo lake lilikuwa ni nini), lakini alisema, "Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka iwe, hivyo ndivyo anavyolifanya." Vema, hiyo ni kweli.

Sasa, ni nani kati yetu atakayemwambia, "Amekosea"? Ni nani atakayethubutu kusimama mbele za Mungu, na kusema, "Umekosea, Bwana, Unapaswa kulifanya jinsi ninavyotaka litendeke, jinsi Dk. Fulani alivyosema linapaswa kufanywa"? Ni nani walio mbali sana katika akili zao, kusema kitu kama hicho? La, usingekuja na kulisema, bali unawazia!

65 Kama vile kwenye Ujumbe wangu wa *Mpinga-Kristo*, "Watatokea makristo wa uongo." Sasa, Yeye hakusema *Mayesu* wa uongo. Mnaona, hakuna mtu angeweza kusimama kimya kuitwa "Mayesu," katika kipindi cha Bwana. Lakini makristo wa uongo maana yake ni "waliotiwa mafuta."

Loo, wao, kila mmoja anafikiri wana upako, "Utukufu kwa Mungu, anaweza kufanya *hili* na kufanya *lile*!" Lakini muweke kwenye jaribio la Neno uone atatokea wapi, mnaona, kwenye Ujumbe wa wakati huu.

Walikuwa na upako katika wakati wa Yesu, bali si juu Yake.

Walikuwa na upako katika wakati … Hata Dathani alikuwa na upako katika wakati wa Musa. Yeye alisema, "Sasa, usifikiri wewe ndiwe pekee uliye mtakatifu miongoni mwetu, Mungu anao wengi. Tutaanzisha tu madhehebu hapa, kundi la watu."

Mungu alimwambia Musa, "Jitenge naye," Naye akaifungua nchi na kuwameza. Alikuwa amempa Musa Neno Lake la asili, nabii Wake; hiyo ndiyo njia pekee aliyowahi kufanya, na njia pekee atakayofanya. Yeye habadilishi mpango Wake, mnaona.

66 Kwa hiyo mawazo yetu ni makosa, mawazo Yake ni sahihi, daima. Wala usijaribu kumwambia kwamba Yeye "amekosea." Haidhuru tunafikiri ni nani anayestahili zaidi, si sisi kusema ni nani anayestahili zaidi. Sasa, hapo ndipo unapoingia katika madhehebu.

Maskini ndugu fulani aliyejazwa na Roho ataenda katika mji fulani na kuunda madhehe-…aunde kundi zu—zuri la watu, nao watakutana mkutanoni, na ndugu wote watakatifu watakuja, unajua, na kusema, "Wajua nini? Naamini maskini Jones hapa,"(yeye kidogo ni mashuhuri miongoni mwao)"Nafikiri anapaswa kupata lile hekalu zuri kubwa, nafikiri. Huoni hilo ni sawa?" La, jamani. Huyo hapo anakwenda. Na halafu kusanyiko linatawanyika. Mnaona? Watenganishe hawa! Mungu ndiye anayetenganisha, Yeye Ndiye anayefanya hivyo. Lakini hao wote, kila mmoja, anataka kumchukua maskini jamaa *huyu*, amweke hapa, na *huyu* amshushe chini. Hilo ni wazo la mwanadamu.

67 Mwanadamu ana funguo, lakini kwa kweli Mungu ndiye aliye na hizo funguo. Wanawapa wanafunzi, kanisa takatifu, funguo; na angalia mara ya kwanza walipolitumia, wakati Yuda alikuwa ameanguka kwa makosa. Walikusanyika na kupiga kura; na ndugu watakatifu. Ni nani angesema hawakuwa ndugu watakatifu? Ni nani anayesema hawakuwa watakatifu? Lakini wao walipiga kura, nayo ikamwangukia Mathiya. Na wakati yeye … Yeye aliwahi kufanya nini? Hakuna kitu. Lakini Paulo alikuwa ndiye mteule! Amina. Hilo lilikuwa ndilo chaguo la Mungu: Myahudi mdogo, mwenye pua iliyopindika, mchokozi, mwenye hasira kali. Si Mathayo, D.D., mwajua, yeye—yeye alikuwa … Ni Paulo. Mungu alimchagua Paulo; kanisa likamchagua—likamchagua Mathiya. Mnaona? Huna haki ya kumwambia Mungu "amekosea." Yeye anajua la kufanya, anajua kile mtu huyo alichotengeneza.

Ni nani angeweza … Kanisa hilo liliwahi kumchagua Paulo? Loo, la, kamwe. Kasema, "Jamaa huyo ndiye anayetufunga sote gerezani."

Lakini Mungu alisema, "Nitamwonyesha yatakayompasa kuteswa kwa ajili Yangu." Yeye alijua nini.

Vema, haidhuru tunafikiri ni nani, Mungu anajua ni nani anayestahili sana kwa sababu anajua moyo wa mwanadamu, Yeye anajua.

68 Wala uamsho, ama mambo haya, hayatukii wakati tunafikiri yanapaswa kutukia. Tunafikiri, "Ni wakati huu sasa hivi, utukufu kwa Mungu!" Ninaona katika matawi yetu na kadhalika ya Wafanyi Biashara, "Kunakuja sasa hivi, haleluya, ufufuo mkubwa!"

Usidanganyike, "Yeye tayari amekwisha kuja, nao wakamtendea yale waliyotaka." Mnaona? Lakini wao wanafikiri kuna uamsho. Unatukia? La! Umekwisha, na umekufa, umeisha. A-ha. Angalia, huu ni wakati wa kutengeneza taa, kutoka na kuingia. "Wale wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya."

69 Angalia hapa katika somo letu, angalia Daudi, mfalme wa Israeli, yeye ndiye aliyepata ufunuo wa kulirudisha sanduku la Mungu mahali pake; ya kwamba, hawakutaka shauri katika siku za Sauli kwa sababu Sauli alikuwa amerudi nyuma. Kwa hiyo hawakutaka shauri kwenye sanduku hata kidogo, lile agano, katika siku za Sauli, maana alikuwa amerudi nyuma na kumwacha Mungu. Kwa hiyo Daudi, upesi, akiwa na uvuvio … Sasa angalia jambo hili, ni somo linalotatiza sana usipolifahamu vizuri. Nami ninahisi ya kwamba saa yaja ambapo tunapasa kuwa watu wazima badala ya watoto wachanga. A-ha. Tunapaswa kula chakula kigumu badala ya maziwa.

70 Angalia Daudi, mfalme wa Israeli, mfalme alikuwa ndiyo kwanza tu atiwe mafuta awe mfalme; ama kuchaguliwa kuwa mfalme, Sauli… Samweli alimtia mafuta kwa mapenzi ya Mungu; naye alikuwa ni mfalme aliyechaguliwa na Mungu kabisa, bila shaka. Naye yuko hapa, na uvuvio unamgusa. Lilifunuliwa kwa Daudi. Alipata ufunuo, hakuna mtu mwingine aliyekuwa amesema lolote juu yake. "Hebu twende tukalichukue sanduku, maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwamba tuwe na sanduku hili hapa, tupate kumtaka shauri Mungu kwa sanduku hili." Jambo la kishujaa sana. Hivi hamwoni hivyo? Vema.

71 Kumbukeni, lakini, yeye akiwa mfalme, na kupokea ufunuo, alitoka mahali pake. Kulikuwako na nabii nchini aliyeitwa Nathani, ndiye aliyechaguliwa kupata ufunuo. Kuna cho chote cha kusemwa, Yeye alisema, "Bwana hatendi neno lo lote mpaka awafunulie watumishi Wake nabii." Lakini, mnaona, Daudi akiwa mfalme, akiwa na upako juu yake … Sasa, hilo ni Maandiko? Akipakwa mafuta, na akapata ufunuo wa kweli; bali ilikuwa ni makosa: Kwa sababu Nathani alikuwa nabii wa wakati huo; wala ufunuo haukumjia Nathani; na wakati ufunuo ulipomjia Daudi, hata hakumtafuta shauri Nathani kuhusu jambo hilo. Yeye ataendelea tu na kufanya yale aliyotaka kufanya. A-ha.

72 Lakini angalia ni nani Daudi alimwuliza shauri hapa katika mlango wa 13, "Lakini aliwataka shauri maakida wa maelfu na wa mamia," akarudi kwenye kusanyiko lake. Mnaona? "Sasa, hivi hudhani tunapaswa kufanya …?" Hilo silo. Sasa, yeye alikuwa akijaribu kumtumikia Mungu, bali hakuamriwa kufanya hivyo; mnaona, maana Mungu alikuwa na njia.

Ni kama tu vile Mungu alivyoweza kunena na—na mfalme juu ya ugonjwa wake na kupona, bali Yeye hakufanya hivyo, alikuwa na njia iliyoamriwa ya kufanya jambo hilo, huyo alikuwa ni nabii Wake. Kwa hiyo Yeye alinena na nabii, Isaya, akamwambia arudi na kumwambia Hezekia kile kitakachotukia.

Sasa, Hezekia alikuwa akinena uso kwa uso na Mungu, na—na Mungu angeweza kuzungumza na Hezekia, bila shaka, bali alifanya njia fulani! Mnaelewa jambo hilo? Mungu ana njia Yake Mwenyewe ya kufanya mambo: kutuma miamsho, kuzungumza, kunena, cho chote kile. Yeye ana njia Yake ya kufanya jambo hilo, nasi si watu wa kumwambia jinsi ya kulifanya. Yeye hulifanya jinsi inavyompendeza kulifanya.

73 Kwa hiyo, mnaona, Daudi, akiwa amevuviwa … Sasa, mnakumbuka nilisema, upako, upako wa uongo? Kumbuka Roho Mtakatifu anaweza kuja na kumtia mtu mafuta, na hata hivyo ni nje ya mapenzi ya Mungu. Hapa, linathibitisha papa hapa. Mnaona? Inatupasa kupitia katika njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo, si njia zetu, njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo. Maana, Daudi, akiwa ni mfalme, ametiwa mafuta, ametiwa mafuta na Roho wa Mungu juu yake (mfano wa Yesu Kristo), lakini hiyo haikuwa ni njia ya Mungu.

Wakati kusanyiko lote, "jambo hilo liliwapendeza," Biblia ilisema. Angalia, maakida wa maelfu na wa mamia, pia makuhani na wanatheolojia walidhani hilo lilikuwa ni la "ajabu." Hizo hapo shule zenu za Biblia na cho chote kile, wao walidhani ilikuwa ni "ajabu sana." Hata watu wote walikubali, na makuhani, na—na wote wakakubali ya kwamba upako wa mfalme ulikuwa sahihi. Angalia! Lakini Mungu hakuwa ameahidi kufunua Neno Lake katika wakati Wake *kwao.* Mungu alikuwa na njia Yake ya kufunua Neno Lake, bali si *kwao*. Kumbukeni, ilikuwa ni kinyume cha Mungu.

74 Kitu kama katika siku za Mikaya mwana wa Imla. Mnakumbuka hadithi hiyo? Yuda na Israeli walitengana, nao walikuwa na falme mbili mbalimbali, naye Ahabu alikuwa ni mfalme wa ufalme mmoja. Na Yehoshafati alikuwa mfalme wa mfalme—ufalme wa Yuda, ninaamini ndivyo ilivyokuwa; naye Ahabu alikuwa juu ya Israeli, Yerusalemu.

Angalia, na halafu hapa likaja kundi la wageni na kuchukua sehemu ya nchi waliyopewa na Mungu ambayo Mungu alikuwa amewapa Israeli, na hawa Wafilisti kule juu, ama Waashuri, walikuwa wakishikilia ardhi hiyo na walikuwa wakiwalisha watoto wao kwa ardhi iliyokuwa mali ya Israeli. Na kwa hiyo walihitaji ardhi hiyo kuwalisha watoto wao wenyewe na familia zao wenyewe. Mungu aliwapa … Hizo zilikuwa ni haki zao walizopewa na Mungu.

75 Na kwa hiyo Ahabu anamwita Yehoshafati, na kusema, "Shuka uje." Akasema, "Angalia kule jinsi adui wetu anavyofanya. Ni haki kwamba sisi, watu wa Mungu, tukiwa na haki tuliyopewa na Mungu kwamba tunapaswa kuwa na nchi hii, ni yetu, Mungu kupitia kwa nabii wake, Yoshua, aliigawa nchi hii, inapaswa kuwa ni yetu; ni mali yetu sisi, ni ya watoto wetu, na hapa wakomunisti wameichukua, nasi tunaninii… Tuna njaa sana, nao wana haki zetu tulizopewa na Mungu. Hivi hamdhani ya kwamba inatupasa kwenda huko na kuirudisha nchi yetu? Kama mtajiunga na vikosi vyenu: kama ninyi Wamethodisti, na Wapresbiteri, na wote, na Wapresbiteri, na Waluteri, na kadhalika, wote watachukua baraza la ekumeni hapa sasa, sote tutaketi pamoja, na tutachukua jambo hilo ." (Ninasema na kunena kwa njia ya mfano sasa.) "Tutakwenda kulichukua."

"Mbona," akasema, "hakika, sisi sote ni mmoja." A-ha.

Sasa, Biblia ilisema, "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana?" Mnaona?

Hapo ambapo huyo mtu mashuhuri, yule mtu mashuhuri wa Kipentekoste, Yehoshafati, alijichanganya

na umati mbaya. Na hilo ndilo lililowapata Wapentekoste wetu leo. Kuna baadhi ya watu halisi mle ndani, bali wamechanganyikana katika kundi hilo la kimadhehebu. Ondokeni kwenye kitu hicho! Ni laana ya Bwana!

76 Angalia sasa! Huyo hapo, naye akasema, "Naam, hilo linasikika la busara." Kasema, "Magari yetu ni yako; watu wetu. Hata hivyo, sisi sote ni Wayahudi. Hakika, tutakwenda pamoja nawe." Lakini je! Dini imesalia tu katika Yehoshafati kusema, "Hivi hamfikirii sisi—tunapaswa kumtaka Bwana shauri kwanza?" Mnaona? "Nafikiri lingekuwa ni wazo zuri."

Mbona, Ahabu, "Bila shaka." Kasema, "Mbona, loo, hakika, ilinipasa kuwazia jambo hilo."

"Vema, kuna mtu wa Mungu mahali fulani? Mna nabii?"

"Aha, nina mia nne yao. Nina baraza zima hapa chini, dhehebu lote. Hao ni manabii wa Kiebrania."

77 Sasa kumbuka, Biblia ilisema wao walikuwa "manabii, manabii wa Kiebrania," si manabii wa makafiri, manabii wa Kiebrania; shule yao, seminari ya kitheolojia.

"Vema, walete!"

Nao wafalme wakavaa na kuketi mbele zake kumvutia nabii. Na huyu hapa anakuja, ninaamini ilikuwa ni Zedekia aliyekuja, yule chifu mkuu wa baraza la wilaya, ama cho chote alichokuwa, akaja pale miongoni mwao. Alijifanyia pembe mbili kubwa, akasema, "Nimesikia kutoka kwa Mungu. BWANA ASEMA HIVI, 'Kwa pembe hizi utawasukuma Waashuri watoke nchini.'"

"Ee utukufu!" kila mtu alifikiri hilo lilikuwa ni zuri sana, sawa.

78 Angalia jinsi linavyokaribia kwenye ukingo huo wa wembe sasa, kati ya mema na mabaya. Na kumbuka itaangukia upande mmoja ama huo mwingine, mpaka wakati mwingine inakuwa kama wembe mkali baina ya tafauti kati ya kweli na uongo. Haina budi kuwa ni kila Neno la Mungu; si karibu kila Neno, bali kila Neno! Na imefikia ambapo leo, si kwa Waluteri, si kwa Wamethodisti, si kwa Wapentekoste, lakini kwenye wakati huo ulionolewa, katika wakati huu ambapo upako wa mpinga Kristo ni mkamilifu sana, hata ingewapoteza walio Wateule, wataangukia upande mbaya kama hawakuangalia jambo hilo, kama kabari. Angalia! Kuwa mwangalifu! Hatuishi katika wakati wa Kipentekoste sasa. Tumepita wakati huo, kama tu vile tulivyopita Lutheran, na kupita … Mnaona?

79 Angalia. Sasa manabii wote walitabiri, mia nne yao, walioshibishwa vizuri, manabii wa Kiebrania waliwashuhudia, kwa nia moja, "BWANA ASEMA HIVI, 'Kweeni, Bwana yu pamoja nanyi.'"

Yehoshafati akasema, "Vema, hilo—hilo linasikika sawa. Lakini," kasema,"una mwingine?"

"Mwingine? Tuna madhehebu yote hapa, tuna baraza zima lililokusanyika hapa. Kwa nini tunahitaji mwingine?"

Akasema, "Aha," kasema, "Nilidhani labda huenda kukawa na mwingine."

Akasema, "Loo, naam, kuna mwingine, bali hata yeye si mfuasi wa baraza hili." A-ha. "Yeye ni mtu aliyetengwa. Ni Mikaya, mwana wa Imla, nami ninamchukia." Mnaona? Kasema, "Hawatampokea katika ushirika, naye kwanza ni mtu aliyetengwa. Naye daima, kila kitu anachotabiri, hataitia moyo seminari yangu hata kidogo." A-ha. "Naye anafanya mambo haya yote maovu, daima anatabiri mabaya juu yangu, ili tu awe tofauti."

"Loo," Yehoshafati akasema, "usimwache mfalme aseme jambo kama hilo. Lakini ningetaka kusikia yale mtu huyu atakayosema."

80 Kasema, "Vema, tutampata." Kwa hiyo wakawatuma mahali fulani nyikani, nao wakamtuma mtu.

Kasema, nikamwambia, kasema, "Sasa, unapokuwa unarudi sasa, ninataka kukwambia jambo fulani. Je! Unataka kurudi katika dhehebu tena?" Mnaona? "Je! Unataka kuwa na ushirika nao wote tena? Kama ukifanya hivyo, sema jambo lile lile mkuu wa wilaya asemalo, sema jambo lile lile asemalo askofu, nao watakurudisha moja kwa moja. Sasa huu ndio wakati wa kufanya jambo hilo."

Lakini je! ungeweza kuwazia nabii wa kweli wa Mungu, aliyetiwa mafuta akipatana katika Neno moja la Mungu? La hasha!

Yeye alisema, "Kama Bwana aishivyo, nitasema tu yale Mungu asemayo!" Tunahitaji mwana wa Imla. "Kama Bwana aishivyo, nitasema tu yale asemayo." Hiyo ni kweli, yale "*Yeye* asemayo."

81 Kwa hiyo walipofika pale mbele za watu, manabii wote, walisema, "Sasa, unasema wao …"

Akasema, "Ngoja, nipe usiku wa leo, hebu nione yale Bwana atakayosema." Kwa hiyo, usiku huo, Bwana alimtokea katika ono na kumwambia la kusema.

Kesho yake asubuhi akasema, "Unasemaje, Imla?" wakati wote walipokuwa wamesimama nje … Namaanisha "Mikaya, mwana wa Imla," kasema, "unasemaje sasa? Sisi sote tuko hapa pamoja, makuhani wote, na manabii wote, na wafalme wote, na kila kitu kinachoketi hapa pamoja. Unasema nini sasa katika baraza hili kuu?"

Kasema, "Kwea," kasema, "bali nimewaona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji."

Naye Ahabu akasema, "Nilikwambia nini! Huyo msaliti anaweza tu kutabiri mabaya juu yangu!"

Angewezaje kusema jambo lingine lo lote wakati Mungu alikuwa akisema jambo lile lile? Nabii anapaswa kuwa kinywa cha Mungu akinena, si mawazo yake mwenyewe. Yake … Mnaona, yeye ana- … amejitolea kabisa kwa Mungu, hataki kuumiza kitu, bali hana budi kusema yale Mungu asemayo, maana yeye mwenyewe hana mamlaka juu Yake. Mnaona?

82 Akasema, "Sasa, si nilikwambia?"

Ndipo basi akaja yule—yule mtu mkubwa mwenye ile pembe, na kumpiga kofi mdomoni, akasema, "Roho wa Mungu alipitia njia gani wakati alipotoka kwangu?" Kwa maneno mengine, hebu nijaribu kulivunja hilo, "Angalia hapa katika … Angalia hapa, ninataka kukwambia jambo fulani, Mikaya. Je! Unatambua ya kwamba mimi ni hodari katika Maandiko? Je! Unatambua ya kwamba nina upako?" Ama, "Ubatizo," tungesema leo. "Je! Unatambua ya kwamba nina huo?"

Imla akasema, "Sitilii shaka hilo."

Yeye alisema, "Lakini sikilizeni! Roho wa Mungu ameniambia, na akashuhudia pamoja na watu wangu wote mia nne hapa, ya kwamba 'tutawasukuma Waashuri watoke nchini.' Na wewe ni nani kuja hapa na kusema ya kwamba mfalme wetu mkuu atauawa?" Yeye alisema, "Roho wa Mungu aliniambia hivyo."

83 Hebu nilifafanue tu ili mpate kulifahamu. Na labda tunamwona Mikaya akisema, "Jana usiku katika ono, bwana, nilimwona Mungu ameketi juu ya Kiti cha Enzi. Nami nikaona jeshi lote la Mbinguni limekusanyika kumzunguka, a-ha, nao walikuwa na baraza Mbinguni. Wakasema, 'Ni nani tunaweza kumtuma ashuke aende akamdanganye Ahabu? Kwa sababu chini ya Kiti cha Enzi hapa kuna nabii, nabii wa kweli, jina lake ni Eliya. Naye ametabiri kwa Neno Langu na kusema ya kwamba "Huyo Ahabu mwovu, kwa sababu alimwua Nabothi, mbwa watairamba damu ya mtu huyo mwovu," nasi hatuna budi kulifanya Hilo litimie kwa sababu tayari limenenwa, ni BWANA ASEMA HIVI! Halina budi kutimia, halina budi kuwapo. Na tutafanyaje jambo hilo?'"

84 "Ndipo chini huko kutoka kwenye maeneo ya kutambaa ya waliopotea, huko chini kabisa akatokea roho fulani anapanda juu, akasema, 'Mimi ni mdanganyifu, na kama ninaweza kuwatumikia, nitashuka niende nikamwingie nabii wake.'" Kwa sababu walikuwa wamejiundia madhehebu sana, wataelewa jambo moja tu, na hilo ni mihemko midogo. "'Nami nitawafanya watabiri uongo. Nami nitamfanya Ahabu awasikilize hao watu mashuhuri badala ya nabii Wako halisi; kwa sababu atachunguza kila kitu asemacho kwa Neno lako, atachunguza maono *yake* kwa Neno, atachunguza kila kitu afanyacho kwa Neno, na kama si kulingana na Neno asingelisikiliza. Lakini kama … Ninaweza kuwadanganya hawa wengine, nami nita … wao … Ahabu ana matumaini makubwa sana katika huo mfungamano wa pamoja wa usalama wao, kwa hiyo wanaenda pamoja kila mahali nao wataungana. Nami nitamfanya Ahabu awasikilize, aende huko nje. Na hivyo ndivyo tutakavyofanya. '"

"Mungu alisema, 'Unaweza kufanya hivyo, wewe ni mdanganyifu kwelikweli; wewe shuka uende.'"

85 Ndipo Zedekia akampiga kofi mdomoni, akasema, "Ulikuwa wapi …?"

Akasema, "Utaona utakapokuwa umeketi kwenye chumba cha ndani." A-ha.

Akasema, "Kwea!" Zedekia akamwambia mfalme. Kasema, "Kwea na urudi kwa amani!"

Ahabu akasema, "Mchukue jamaa huyo ukamweke gerezani. Mweke katika pingu, mlishe chakula cha shida na maji ya shida. Na wakati nitakaporudi na ushindi wangu kutoka hapa nje, ambapo manabii wangu wameniambia ya kwamba 'ufufuo huu hauna budi kutukia,'" kasema, "Jamaa huyo atanitambua!"

Sikiza maneno ya mwisho ya Mikaya kwa mtu huyo: "Ukirudi kabisa, basi Mungu hakunena nami." Loo!

Mnaona, Mungu ana njia Yake ya kufanya mambo. Watu hawa walidhani walikuwa wakimtumikia Mungu. Kuwa mwangalifu! Si mhemuko, si shauku, si mawazo, bali halina budi kuwa "BWANA ASEMA HIVI," halina budi kuwa ni kweli. Vema, haidhuru … Tunaona mambo haya kuwa hivyo.

86 Angalia sasa wakati Daudi alipotoa tangazo hili kuu, na ilionekana kana kwamba lilikuwa ni zuri, jambo zuri kufanya. Ndipo tunaona ya kwamba … (Ninawachosha? Je! Nimechelewa sana kupata mwingine?) Walikuwa wametoa tangazo hili kuu, hakumtafuta shauri nabii.

Sasa, kila mtu anajua ya kwamba Amosi 3:7 ilisema ya kwamba Mungu aliahidi ya kwamba kamwe

hatafanya lolote mpaka kwanza amfunulie nabii Wake. Kupitia nyakati za kanisa tumekuwa na watengenezaji; lakini aliahidi kwa Malaki 4 ya kwamba kungekuwako na nabii nchini katika siku za mwisho (kwa sababu haina budi kuendana na utaratibu huo, mnaona) kabla ya wakati wa mwisho kuja.

87 Kabla ya kuja kwa kwanza kwa Yesu, Eliya alikuja, Eliya wa Malaki 3. Mathayo 11 inasema hivyo, "Kama mnaweza kufahamu hilo, huyu ndiye aliyenenwa habari Zake, 'Tanzama ninamtuma mjumbe Wa—Wangu mbele Zangu.'" Sasa, Yeye ametabiriwa, wanatheolojia wote wanaamini jambo hilo; ya kwamba, katika siku ya mwisho, Roho wa Eliya atakuja, pia. Hana budi kuja mara tano, Mungu anatumia Roho huyo: Elisha, Eliya, Yohana Mbatizaji, na kwa ajili ya kanisa la Mmataifa, halafu kwa Wayahudi katika Ufunuo mlango wa 11. Hiyo ni, n-e-e-m-a ya Mungu, i-m-a-n-i, J-e-s-u-s, Yesu, he—herufi tano. Huwezi kusimama kwenye nne, haina budi kufikia tano. Mnaona? Angalia!

88 Sasa, Yeye aliahidi jambo hilo, kwa hiyo hilo linaiweka Biblia kwenye siku hii hasa, na Sodoma na Gomora. Naye Eliya hakuwa … Huyo hakuwa Eliya; Huyo alikuwa ni Roho wa Mungu juu ya Eliya; Eliya alikuwa mwanadamu tu. Sasa, tumekuwa na akina Eliya, na makoti ya Eliya, na majoho ya Eliya, na kila kitu cha Eliya. Lakini Eliya wa siku hizi ni Bwana Yesu Kristo. Yeye atakuja kulingana na Mathayo wa kumi na saba … Luka 17:30, inasema Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Si mwanadamu, Mungu! Lakini itakuja kupitia kwa nabii. Sasa, Yeye kamwe hakuwa na manabii wawili wakuu kwa wakati mmoja, kamwe, ulimwenguni. Mnaona? Haidhuru ni kiasi gani kuna … vichwa viwili—viwili haviwezi … Haina budi kuwa kichwa kimoja. Mungu hana budi kumweka mtu mmoja chini ya mamlaka Yake. Mnaona? Kuna Mungu mmoja; kulikuwako na Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, bali Mungu mmoja juu ya yote, angalia, na akatumia tu afisi hizo. Vivyo hivyo na Yeye pamoja na Eliya, Roho wa Eliya; alitumia Roho huyo, lakini Mungu yeye yule akimtawala wakati wote kutimiza Neno Lake.

89 Sasa, angalia katika jambo hili sasa, Daudi alifikiri alikuwa na kila kitu katika utaratibu. Naye alikuwa amevuviwa. Mnaona jinsi Roho Mtakatifu anavyoweza kumtia mtu mafuta? Lakini haina budi kuwa katika kanuni ya kutia mafuta. Roho ya nje inaweza kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu, na nafsi iwe nyeusi kama lami. Gugu linakua kwa maji yale yale yanayokuza…yanayoweka uhai katika ngano, yanaweka uhai katika gugu; lakini ndani kabisa ya gugu, ni uhai wa gugu. Ni kushangilia, na kuchanua, na kupata uhai, na kufanya kila kitu ambacho ngano hufanya, bali nafsi yake ni *gugu*. Mnaona? Waalimu wa uongo wanaweza kuinuka, wakifundisha kila namna ya utatu na chochote kile, na kutiwa mafuta na Roho Mtakatifu, na kufanya miujiza mingi tu kama Injili ya kweli inavyoweza. Lakini kwa Neno hapa, hilo ndilo linalofanya jambo hilo. Mnaona ninalomaanisha? Sasa, ni sawa kufundisha jambo hili, nadhani, mimi—mimi niko katika maskani ya madhehebu mbalimbali asubuhi ya leo, katika—katika hoteli hii hapa.

90 Angalia, angalia yale tunayosema. Sasa, vema, sikilizeni. Daudi alikuwa na mhemko wote ambao ufufuo halisi ulikuwa nao. Angalia! Walipiga makelele, walipaza sauti, walicheza, kwa kweli walipata kitu fulani kutokana na upako huo. Hakika walifanya hayo! Yote kama tu ufufuo halisi, lakini, unaona, Mungu hakuwa ndani ya huo. Mungu hakuwa ndani yake. Alikuwa na nabii ameketi papo hapo nchini. Walipaswa kujua. Mnaona? Daudi alipaswa kujua jambo hilo.

Kitu fulani siku hizi, tuna mitambo yote, kama vile madhehebu makuu, mikutano ya hadhara ya wakati wetu, bali matokeo yake yanakuwa kama yalivyokuwa wakati huo; matokeo yetu ya mikutano yetu mikubwa, na sababu zetu zote kubwa nzuri, majengo yetu makubwa, na ninii yetu kubwa … kujenga maelfu, na kuongeza washiriki na kadhalika, inakuwa vivyo hivyo, yote ni marudio. Sisemi jambo hilo kuwa tofauti, ninasema jambo hilo kuwa mwaminifu mbele za Mungu, ambaye ninasimama karibu na Kitabu Chake asubuhi ya leo. Mnaona? Yote yanatokea kuwa ni bure, matokeo yale yale.

91 Sasa hebu na tuone ilivyokuwa wakati Mungu (katika majira na wakati Wake) na manabii wake wanapopuuzwa, kutegemea tu theolojia, makasisi, umadhehebu kama tunavyofanya siku hizi. Sasa, kwa makini. Yote yanachafuliwa. Kama Roho wa kweli wa Mungu pale, atalielekeza katika Neno; si mahali pamoja tu katika Neno, Neno lote kwa wakati wote. Mnaona?

Siku ya Pentekoste, Roho alilielekeza moja kwa moja katika Hilo, kwenye Yoeli 2:38. Mnaona? Siku za Luther, alilielekeza moja kwa moja kwenye Hilo; Wesley; katika mwenendo huu wa mwisho wa kipentekoste; lakini huu ni wakati mwingine, huku ni kuitwa kwa Bibi-arusi atoke. Si miaka elfu mbili iliyopita kwenye Pentekoste, ama kurudiwa, ama kule kurudi. Pentekoste …

92 Roho Mtakatifu alikuwa katika Luther, Roho Mtakatifu alikuwa ndani ya Wesley; ni Neno la Mungu likitiwa mafuta. Naye Roho Mtakatifu akarudi kwa watu wa wakati huo na wakaanza kupata kurudishwa kwa karama. Waligundua, kwa kujitolea wenyewe kwa Mungu, Roho Mtakatifu alinena kwa lugha kupitia kwao. Waliweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao wakapata afya. Walicheza katika Roho. Mnaona? Huo ulikuwa ndio wakati wa matengenezo kulirudisha kanisa katika utaratibu. Na utaratibu wa mwisho wa kanisa ulikuwa ni kuweka karama kanisani; kama vile Luther alivyoweka kuhesabiwa haki, Wesley aliweka utakaso, Pentekoste iliweka vipawa. Lakini walifanya nini? Kosa lile lile, kama vile maumbile yamefananishwa na shina la ngano, waliunda madhehebu (ambayo ni kinyume cha Mungu, kinyume cha Mungu).

93 Sasa, tunaona ya kwamba wakati … Ndipo shina hili litakapokusanyika pamoja, wanaunda wazo lao wenyewe. Na haidhuru … Wakati ile "hoja mpya," kama wanavyoiita, walipotoka kwenye Assemblies of God, walifanya nini? Wasingeweza kulipokea. Haidhuru ilikuwa ni Kweli kiasi gani, ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, tayari walikuwa Baraza Kuu. Mwanadamu tayari alikuwa amechukua mamlaka, Roho alikuwa tayari amewaacha. Sawa! Na ndipo jambo hili likatokea … Nimezungumza na baadhi ya viongozi wenu bora; wanasema, "Vema, tungefanyaje sasa?" Wangejionea aibu. Wakati, wanajua ni Kweli; wasipofanya hivyo, wao ni vipofu kiroho na hawajui Biblia. Si kwamba nasema jambo hilo kwa ubaya, sasa, nasema hilo kwa uchaji. Maana, hakuna mahali katika Biblia ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa kwa kutumia vyeo hivyo, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Wala haukutumika mpaka baada ya baraza la ekumeni, kanisa Katoliki la Kirumi. Katekisimu yao wenyewe inashuhudia jambo lile lile. Ni fundisho la sharti la Katoliki! Si fundisho la Biblia, bali fundisho la sharti la Katoliki. Na ninyi Wamethodisti mkaleta katekisimo zenu na kila kitu kama tu walivyokuwa nazo, zikikua pole pole. Lakini sasa wakati ulipokuja kwenye Pentekoste, na kueneza baadhi ya mafundisho hayo ya sharti, ungali uliyashikilia.

Lakini sasa ni kuitwa kwa Bibi-arusi, sasa ni wakati ambapo Mihuri Saba imefunguliwa, sasa wakati yale mambo makamilifu ambayo watengenezaji waliacha yatafunguliwa; na Malaki 4 tu ndiyo inayoweza kufanya jambo hilo, kwa sababu inachukua ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu hadi kwa mtu binafsi kufanya jambo hilo. Hiyo ni kweli! Hauwezi kulijia kundi, haijatukia kamwe. Mtu mmoja! Hivyo ndivyo Mungu alivyoahidi katika vivuli vya kuja kwa Bibi-arusi Wake, Eliezeri. Mnaona?

94 Angalia wakati makuhani, wahudumu, na kadhalika, wanapopata uvuvio wao wenyewe, na kutiwa mafuta kweli. Daudi alitiwa mafuta. Biblia ilisema hivyo. Lakini, mnaona, alipitia kwenye chanzo kisicho sahihi, alienda kwenye njia mbaya. Yeye alielekeza upako wake upande mbaya, kwa watu na yale waliyowazia, kwa maakida, yale waliyowazia, badala ya njia ya Mungu takatifu kutafuta kujua BWANA ASEMA HIVI, "Je, huu ndio wakati wa hili? Je, huu ndio wakati wa jambo hili? Haya ni mapenzi ya Mungu?"

95 Basi kama yeye ni nabii wa kweli wa Mungu, atatangulia mbele za Mungu, aseme, "Baba, ni kitu gani?" kama vile Nathani alivyofanya baadaye kwa Daudi.

Daudi alisema, "Je! ni vizuri mimi kuishi katika nyumba ya mwerezi, na sanduku la Mungu wangu linakaa chini ya mahema huku nje?"

Na mwangalie Nathanaeli, kasema, "Daudi, fanya yote yaliyo moyoni mwako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe. Wewe ni chombo kilichotiwa mafuta cha Mungu."

Lakini huyo akiwa ni nabii, na kosa lake, na wajibu wa Mungu kwa nabii Wake. Usiku huo Yeye alimtokea, akasema, "Enenda, ukamwambie mtumishi wangu Daudi, ninapenda ujasiri wake, ninampenda kwa ajili ya jambo hili, maana yeye ni mtu anayeupendeza moyo Wangu, na ninajua wakati umewadia kwa sanduku langu kuwa hivyo, kuwekwa chini na kitu fulani, lakini mimi ninaninii tu… Si majira yake ya kutukia. Nitamwacha mwanawe afanye hivyo, lakini sitamruhusu afanye hivyo."

Ndipo huyu hapa Nathani anakuja na, "BWANA ASEMA HIVI, Daudi, ule ufunuo mkuu uliokuwa nao ni makosa kama ulivyokuwa ulipoleta lile sanduku." (A-ha! A-ha! Mnaona?) "Usifanye hivyo. Usijaribu! Bali Mungu alisema Yeye atamtaka 'mwanao afanye hivyo.'" Pale! Mnaona? Haya basi!

96 Daudi alitiwa mafuta kusema jambo hilo kwa sababu hapo awali angeweza kuliona, kama tu vile Ibrahimu alivyotafuta Mji duniani. Mnajua, alikuwa akiutafuta kwa sababu yeye alikuwa yuaenda kuishi hapa siku moja, Ibrahimu ataishi hapa, katika Mji huo. Naye akazunguka-zunguka akiutafuta. Na papo hapo kwenye misingi ile ile ambapo aliangalia, ilikuwa juu yake basi, na atarudi katika ule Utawala wa Miaka Elfu naye ataishi katika Mji huo. Lakini akiwa ni nabii, alichaguliwa na kuvuviwa, alijua kulikuwa na Mji mahali fulani, naye alikuwa akiutazamia. Lakini, mnaona, ufunuo wake wote ulikuwa umefichwa kwake. Haikuwa kwa ajili ya umri wake. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] … Kuendelea hadi kwa Yohana, ambapo aliuona ukishuka kutoka kwa Mungu Mbinguni. Huo ulikuwa ndio ule Mji.

97 Mnaona, kila kitu hakina budi kuwa katika majira yake. Unapanda ngano yako katika majira ya kuchipua na … ama katika majira ya kupukutika majani na kuikata msimu ujao wa kiangazi. Mnaona? Haina budi kupanda kupitia kwenye shina, kisha kuja kupitia kishada, na kapi, na kuendelea kuingia … Haina budi kuwa katika majira yake. Maumbile yote yanaendelea katika mwendelezo. Roho wa Mungu aliumba maumbile, na yote Mungu na maumbile yako katika mwendelezo. Mambo yote yaliyowekwa hekaluni yalikuwa ni mfano wa yale aliyoona Mbinguni.

98 Unaona mti ukijitahidi kujaribu kuishi, hiyo inamaanisha kuna mti usiokufa. Ukimwona mtu akihangaikia maisha, inaonyesha ya kwamba kuna maskani yanayongoja mahali fulani ambayo hayafi. "Kama maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa tunayo moja inayongoja tayari." Baba mwema wa Mbinguni aliniruhusu kutembea nyuma ya pazia hilo siku moja na kuliona. Ni wangapi waliosikia ninii …? Mnaona? Kuangalia kulipita pazia la wakati. Hapo hapo ni kama tu ninavyowahubiria ninyi nyote, hao hapo wamesimama. Nafsi zilizo chini ya madhabahu, zikilia, "Hata lini?" Si hadithi tu, mtu fulani aliyekuwa na akili: "Hata lini,

Bwana?" Mnaona? Wakati tunapohisi jambo hilo sasa, kama wakati wetu, kama Ndugu Bill Dauch anayeketi hapa kwenye umri wa miaka tisini na mitatu. Kuna kitu fulani kinachomtamani huyo kijana mwanamume, tena. Kuna kitu fulani … Ungetoa chochote. Jinsi ningetaka. Ndugu Jack, na sisi wengine wote. Rudi, Ndugu Gerholtzer, humu ndani, katika huo ujana. Tunataka kufanya jambo hilo kwa ajili gani? Kuwa kijana na kuzurura tena? La, bwana! Kwa sababu tunajisikia tungekuwa na wakati zaidi wa kumtukuza Mungu huyu tunayempenda.

99 Na ndugu zangu wapendwa, nina Ujumbe huu asubuhi ya leo, kuna Nchi ng'ambo ya mto wanayoiita hiyo tamu milele. Hapo tutamtukuza Yeye katika nyakati zote, na nyakati zote, na Umilele. Kwa nini tunajisikia hivyo? Kwa sababu kilindi kinaita kilindi. Na mradi tu kilindi kinaita, hapana budi kuwe na kilindi cha kuitikia wito huo la sivyo kusingekuwako na wito. Kabla ya kuweko na uumbaji, hapana budi kuwe na Muumba kwanza kuumba uumbaji, la sivyo … Hiyo inaonyesha ushahidi wa kweli kwamba yuko.

100 Angalia makuhani hawa, wote wako nje ya mstari. Angalia upako, vema, upako hauna kasoro. Vivyo hivyo na ninyi Wapentekoste, lakini angalieni ni njia gani mnayoingia sasa. Siku imebadilika tangu Pentekoste, jambo lingine kwetu. Kama kusingekuwako na nabii nchini, labda Daudi angekuwa sahihi. Hiyo ni kweli. Lakini hapo alisimama Nathani, amethibitishwa, amechaguliwa, akishuhudiwa na Mungu kuwa nabii.

Angalia! Sanduku katika Biblia daima ni mfano wa Neno kwetu, kwa sababu lilikuwa ni Neno la Mungu ndani ya sanduku. Na alikuwa … Angalia sanduku walilolileta, angalia vile walivyofanya jambo hilo. Halikuwekwa katika hali yake ya asili iliyoamriwa na Mungu. Sasa, Mungu alisema nyuma hapa katika Torati kwamba halina budi … jinsi linavyopaswa kufanywa, jinsi sanduku hili linavyopaswa kubebwa, na kwamba libebwe na nani. Lakini Daudi, chini ya upako wake …

101 Ndugu yangu, usikose jambo hili. Na dada zangu, ninyi mnaotaka kuwa wahubiri wanawake na kadhalika, msikose jambo hili. Haidhuru upako wako ni kiasi gani, huna budi kuingia katika nafasi iliyoandaliwa na Mungu. Upako wa Daudi ulikuwa ni sawa, lakini katika kufanya jambo hilo yeye alishikwa na hisia kali na akavuka mpaka. Alifanya nini? Alivuka mpaka. Badala ya kuliweka lile sanduku mahali pake pa asili, alilibeba kwenye gari jipya na si juu ya mioyo ya Walawi. Ilipaswa kubebwa kwenye mabega ya Walawi, ambayo ni juu ya moyo. Neno haliko mawazoni, limo moyoni! "Si kwenye gari jipya." Hiyo ilikuwa ni nini? Baadhi … Iliwakilisha kitu kipya, Daudi alichofanya pale, alinena habari za kila madhehebu ambayo yatakayotokea. Neno la Mungu halipaswi kuchukuliwa na … kubebwa na wazee wa jimbo ama maaskofu, na kadhalika, wa madhehebu. Ni Ubatizo wa Roho Mtakatifu katika moyo wa mwanadamu, na si katika mwenendo fulani wa kikanisa. Roho Mtakatifu ni hazina ya upendo wa Mungu katika moyo wa wanaume na wanawake kutii. Mnaona?

102 Lilikuwa juu ya mabega ya wahudumu Wake, wahudumu Wake walikuwa ni Walawi. Waliliweka juu ya bega lao la kushoto na kulibeba hilo sanduku namna hiyo, kwa sababu lilikuwa juu ya moyo wao. Walikuwa na mzigo wa Neno mioyoni mwao. Amina! Sasa una mzigo wa madhehebu yako moyoni mwako, mzigo wa kusanyiko lako: kama utajenga *hili*, ama kufanya *lile*, ama kufanya jambo lingine. Ule mzigo wa ni wangapi zaidi mtakaowafikia madhehebu yenu; badala ya mzigo wa Neno la Bwana, mpaka watu wataliona tu Neno la Mungu wala si kitu kingine. Lakini mmelipata kwenye gari jipya sasa. Mnaona? Wao wanalipeleka hapa katika baraza la ekumeni hata, kwenye mabega. Sitaki kukosoa, na Mungu na anisaidie sasa. Ninawaambia tu Kweli.

103 Sasa, wakishawishiwa na kanuni za imani na mabaraza ya ekumeni, lile Neno, Neno halisi la majira ya wakati huo lilipuuzwa, kwa sababu walikuwa na msisimko sana. Lakini Daudi, *mfalme* aliyetiwa mafuta … Yeye alikuwa mfalme, bali alikuwa ametiwa mafuta kuwa mfalme. Unasema, "Mimi ni mhudumu, aliyetiwa mafuta." Basi dumu ukiwa mhudumu, usijaribu kuwa nabii. Mnaona? Kama wewe ni mwinjilisti, dumu mwinjilisti.

Kumbukeni Uzia, katika siku za Isaya, yule mfalme kijana … yule nabii kijana. Uzia alikuwa mtu mashuhuri, mtu aliyetiwa mafuta, Mungu alimbariki; alijibariki. Naam, niliwahubiria jambo hilo hapa wakati mmoja. Na siku moja aliinuka sana hata akafikiri angeweza tu kuchukua ofisi ya kuhani, naye akauchukua ule moto akaingia mbele za Bwana. Na ninii … Hao makuhani walimwambia, "Usifanye hivyo, Uzia!" Lakini yeye alijiinua. Nabii hakuweza kumwambia chochote. Makuhani walijua utaratibu wao, walikuwa wakitimiza utaratibu wao, yeye alisema, "Hilo si agizo lako, Uzia. Usifanye hivyo, hilo!"

104 Vema, aliwafanya "Nyamazeni!" Naye akaenda pamoja na—na ule moto, akaingia kutoa sadaka, akachukua kazi ya kuhani; alikuwa ametiwa mafuta kuwa mfalme, si kuhani. Na hao makuhani walikuwa wakijaribu kumwambia, "Wewe ni mfalme mzuri sana, umetiwa mafuta, Mungu ametubariki sisi vizuri. Lakini wewe ni mfalme, si kuhani."

Nanyi wachungaji kamwe msimwambie nabii la kufanya, au ninyi wainjilisti mmwambie mchungaji. Mnaona, kila mmoja ana ofisi yake kama imetambulishwa kikamilifu.

Kwa hiyo akaingia pamoja na ule moto, naye akapigwa kwa ukoma akafa.

105 Sasa huyu hapa Daudi, mfalme. Daudi anajaribu kufanya jambo lile lile hapa. Yeye amelichukua. "Vema, hilo ni sawa, sina budi kuondoka. Waangalie watu kote. Unasemaje, kapteni? Una elfu kumi."

"Utukufu kwa Mungu, Daudi, ninamsikia Roho." Loo, alifanya hivyo! Yeye aliisikia. "Unafikiri nini, Daudi? Unamhisi?"

"Utukufu kwa Mungu, Yote yako juu yangu! Hebu na tulichunguze tuone kama ni kweli, hebu tuone. Sanduku ni la wapi?"

"La kwetu! Ni mali yetu."

"Tunapaswa kushauriana na nani? Hakika, sanduku. Jambo lile lile tu kama shamba hilo lilikuwa ni la—la Israeli badala ya Wafilisti. Hiyo ni kweli. Ni mali yetu. Na ni kama vile ninavyosikia upako, pia."

Wakuu wa mamia, kusanyiko lote, "Utukufu kwa Mungu!" Walipiga makofi, nao wakapiga makelele, nao wakacheza, na kuruka-ruka.

Walikuwa na Roho, lakini unafikiri Baba alikuwa akiwaza nini? "Jinsi ambavyo nimemtuma Nathani, yule nabii kule chini! Wanajua la kufanya, na vivyo hivyo na Daudi, lakini sasa yeye amechangamka kabisa na kuvuka mpaka wake na akaenda kufanya jambo *hili*."

106 Vema, angalia, "kulibeba mabegani" ulikuwa ni mpango wa asili wa Mungu. Kuna *lazima* tano. Ninawatakeni myaandike haya, kama mna … Ninaona mnaandika.

Na ni dakika ishirini, dakika ishirini na kitu baada ya saa kumi, kwa hiyo nitajaribu kumaliza ifikapo saa kumi na moja, ikiwezekana. Nitaharakisha upesi niwezavyo.

Haidhuru mtu anamfanyia Mungu kazi kwa uaminifu jinsi gani, haidhuru ni mwaminifu jinsi gani, ametiwa mafuta kiasi gani, ni Mpresbiteri namna gani, Mbatisti, Mpentekoste; haidhuru kama wewe ni askofu, shemasi, hata uwe nani, mchungaji, mwinjilisti, nabii, ye yote uwezaye kuwa; kuna lazima tano ambazo hazina budi kufikiriwa kwanza. Haidhuru ni upako kiasi gani, ulionekana ni mzuri jinsi gani, jinsi watu wanavyopiga makelele, kila kitu anachofanya Roho, kuna *lazima*.

107 Sasa, ndugu zangu, wakati mnapoandaa karatasi yenu, mnaweza kuelewa sasa ni kwa nini? Sasa kumbukeni, nyote mmefikiria, na mmefundishwa miongoni mwenu, si … (ona, ninazungumza kote nchini) … ya kwamba sikuamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini katika kunena kwa lugha, bali bado unaweza kunena kwa lugha na usiwe na Roho Mtakatifu. I Wakorintho 13, inasema, "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, bado si kitu." Mnaona? Huo ni upako wa Roho Mtakatifu, ambao hauhusiani na nafsi iliyo ndani yako. Unaweza kunena kwa lugha na kulikana Neno. Nimeona jambo hilo likifanywa, nanyi mnaliona pia. Mnaona? Mwanamke anaweza kuhubiri Injili na … Mnaona? Wanaweza kufanya yote … Wao hukata nywele zao, na wangali wanapiga makelele na kunena kwa lugha na cho chote kile. A-ha, hiyo ni kweli kabisa. Huna budi kujipanga na Kweli ya Neno.

108 Angalia! Haidhuru mtu ni mwaminifu jinsi gani, haidhuru anatumiwa na Mungu jinsi gani, haidhuru yeye ni nani, hana budi kuwa hivi: hana budi… Jambo analonena ni lazima liwe kwa wakati unaofaa kwa Biblia. Mtu fulani anasema, "Vema, Musa kule nyuma." Ninajua yale Musa aliyofanya, bali si yale Mungu anayofanya siku hizi. "Vema, huko nyuma, miaka thelathini iliyopita, Luther alisema …" Hilo huenda likawa ni zuri, bali hilo silo analofanya leo. "Vema, miaka arobaini iliyopita, Pentekoste ilianguka." Lakini hilo silo analofanya leo. Mnaona? Lazima iwe ni ya wakati unaofaa.

Haina budi kulingana na Maandiko. Haina budi liwe katika majira yake, pili. Tatu, na lazima iwe kulingana na jinsi Neno la Mungu lilivyosema ingekuwa.

109 Nawe unasema, "Utukufu kwa Mungu! Roho Mtakatifu alishuka juu yangu, haleluya, kama tu vile alivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste." Lakini hilo huenda likawa ni tofauti leo. Alishuka juu ya Daudi, pia, sivyo? Hakika, alishuka. Alishuka juu ya Uzia, lakini ilikuwa ni makosa! Mnaona, huna budi kuingia ndani zaidi ya hilo sasa. Mnaona? Huna budi kuingia ndani zaidi ya hapo. Sasa, msijisikie kuumia, i—iweni tu na kicho.

Na angalia, na pia haina budi kumjia mtu aliyechaguliwa na Mungu. Si chaguo la kimadhehebu, si la watu kuchagua, bali kulingana na chaguo la Mungu. Na kama ni ujumbe kutoka kwa Mungu, wa ufunuo mkuu kutoka kwa Mungu, hauna budi kumjia nabii Wake. Sasa, kama unataka Maandiko ya jambo hilo, ni Amosi 3:7. Mnaona? Sasa, haina budi.

Kuna mambo matano ambayo hayana budi kuwa: Ni lazima iwe katika wakati wake. Haina budi kuwa ni wakati ambao Mungu alisema ingekuwa. Haina budi kuandikwa katika Neno la Mungu. Haina budi kuwa katika majira ya wakati wa Mungu, mnaona. Na lazima iwe kwa kuchagua kwa Mungu.

110 Na Mungu hahitaji ye yote wetu kufasiri Neno Lake, Mungu ndiye anayejifasiria Mwenyewe. Yeye hahitaji seminari zetu. Yeye hahitaji hekima yetu, ni upuuzi. Mnaona? Hawa alipata hilo, a-ha, na akakosa

ile Fasiri kwa hekima yake.

Sema, "Loo, jamani, jamaa huyo ni mtu mwerevu." Vema, hilo halimaanishi kitu. Hakika. Ahabu alikuwa mtu mwerevu. Belteshaza alikuwa mtu mwerevu. Shetani alikuwa mjanja sana na mchafu, mwerevu, hakuna hata mmoja wenu angeweza kumshinda, hakuna hata kidogo.

Mimi simtegemei … hamna … sina hekima, namtegemea tu Mungu. Mnaona? Mungu yukoje? Yeye ni Neno. Halafu basi Mungu hulifasirije Neno Lake Mwenyewe? Sikilizeni kwa makini sasa, msikose mambo haya. Mungu hulifasirije Neno Lake Mwenyewe? Kwa kulifanya litimie, si moja tu hapa, bali yote kwa ajili ya majira hayo.

Si kusema, "Nuhu toka uende ukahubiri," mwenye uvuvio, lakini, "Jenga safina, iwekee milango, uijenge *hivi*, na *vile*." Vipi kama angeweka mlango juu badala ya chini? Vipi kama aliweka dirisha chini, mlango juu? Mnaona? Haina budi kufundishwa kulingana na wakati, kwa sababu hilo ndilo hasa Mungu atakalolitumia. Haina budi kuwa hivyo, na haina budi kuja kwa uvuvio.

111 Nilimsikia jamaa mmoja akisema wakati mmoja, kasema, "Ninaamini mtu huyo huwaombea wagonjwa, ninaamini ni sawa. Lakini kama kwamba ni nabii," kasema "ninaamini yeye ni nabii wa Mungu; bali kama mwalimu, mbona, yeye ni 'Yesu pekee.'" Ni ninii … Ungemwita mtu wa aina gani huyo? Mtu hajui anachozungumzia.

Neno lenyewe *nabii* linamaanisha kwamba "Yeye ni mfunuzi wa Neno la Mungu," fasiri huja tu kwa huyo. Na hiyo ndiyo sababu siku hizi tuna haja sana na mtu huyu mkuu ambaye anapaswa kutumwa kwetu katika namna ya nabii Eliya, kwa sababu itakuwa ni ufunuo wa Mungu ukijulishwa kwetu kwa kuthibitishwa, ikionyesha ya kwamba ni siku na saa na majira ambayo Mungu aliahidi jambo hilo litakuwa. Na, kumbukeni, atashutumiwa; daima imekuwa hivyo, daima itakuwa. Amekataliwa, kama vile tu kapi litakavyovuta … Kwanza atakubaliwa, kwa sababu kapi huishikilia tu ngano mpaka iweze kufikia jua. Pentekoste itausitiri tu Ujumbe, kuupa mlango uliofunguliwa mpaka utakaposambazwa, ndipo gugu litakapoondoka, nayo ngano itakaa katika Uwepo wa Mwana, mnaona, ipate kuiva.

112 Hakutakuwako na dhehebu lo lote, kumbukeni tu. Ndugu Jack hapa ni mwanahistoria, wengi wenu hapa ni wanahistoria. Hakujakuwa kamwe na uamsho ila yapata miaka mitatu baada ya uamsho walianzisha dhehebu juu yake. Hiyo ni kweli? Na muujiza huu mkuu wa mwisho wa mwenendo wa Mungu katika siku hizi za mwisho, umeendelea miaka ishirini; na uko maili milioni moja kutoka kwa madhehebu, daima unazidi kwenda mbali; kapi linajiondoa, hakuna ushirikiano, hakuna uhusiano wo wote Nalo. Mnaona? Daima hujiondoa Kwake. Hakuwezi kuweko na wengine, ni ngano sasa. Lakini sisi ni wabichi sana. A-ha. Hiyo ni kweli. Inanibidi kukaa katika Uwepo wa Mwana upate kutakaswa, hivyo tu. Wabichi sana; hatuna unyofu, utakatifu, jambo ambalo tunalopaswa kuwa nalo kati yetu, kujua ya kwamba Roho wa Mungu aliye hai, akitenda kazi katika Neno Lake na badoanatuonyesha mambo.

113 Tuna waigaji wa uongo wanaoinuka. Hilo litafanya nini? Kudanganya. Biblia ilisema wangefanya hivyo. "Kama vile Yambre na Yane walivyompinga Musa, vivyo hivyo hawa katika siku za mwisho." Mnaona? Wanafanya jambo lile lile, wanakuja moja kwa moja wakiiiga, hasa kabisa. Mnaona? Kuwa mwangalifu! Angalia Mafundisho ya Biblia. Angalia ujumbe unaofuata ishara hizo! Ingali ni itikadi ile ile ya kale ya ujumbe? Sahau!

Mungu alituma miujiza na ishara kuvutia usikivu wa watu Wake. Wakati Yesu alipokuja tu akiwaponya wagonjwa na kadhalika, vivyo hivyo na manabii. Walifikiri, "Loo, utukufu, Yeye yuaja, Yeye atakuwa Farisayo. Yeye atakuwa Msadukayo."

Lakini Yeye alisema, "Enyi kizazi cha uzao wa nyoka na majoka." Kasema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, kazi zake mtazifanya." Kasema, "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu." Yeye hakulielezea. Haikumlazimu kulielezea. Haleluya. Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya msimu mwingine. A-ha. Yeye alisema tu yale aliyopaswa kusema, "Daima mimi hufanya jambo hilo linalompendeza Baba, na hilo ni kutimiza Neno Lake. Kama silitii, maisha Yangu na kazi Zangu havilingani na Neno Lake ninalopaswa kufanya, basi msiniamini, Mimi si Yeye; lakini kama vinalingana, basi aminini hizo kazi kama hamwezi kuniamini Mimi," akasema.

Angalia sasa haya hayana budi kufanywa.

114 Sasa, mnaona, Mungu hakuwa amewafunulia jambo hilo kwa njia Yake aliyoiandaa, alikuwa ameifunua kwa uvuvio, bali ilikuwa katika njia mbaya. Mnaona, uvuvio utakuwa ni sawa, lakini kama uko kwenye njia mbaya, utapelekwa vibaya. Kama vile ukichukua risasi na kuilenga moja kwa moja kwenye shabaha, inaelekea moja kwa moja kwenye shabaha, lakini mpulizio wa upepo unaweza kuipindisha vibaya. Sasa, katika motokaa yako, ukiendesha barabarani kwa maili sitini, sabini kwa saa na mpulizio wa upepo unakupulizia, unaweza kunyosha magurudumu yako, uyarudishe barabarani tena. Lakini huwezi kupiga risasi; hakuna kitu pale cha kunyosha magurudumu yake, inakosa shabaha. Mnaona, haina budi kusafiri katika njia yake ya asili.

115 Vivyo hivyo Neno la Mungu halina budi kusafiri katika njia Yake ya asili. Hakuna mpulizio mdogo wa upepo utakaoliondoa, hakuna madhehebu madogo yatakayoliondoa, hakuna mateso madogo yatakayoliondoa, limeelekezwa kwenye shabaha! Litapiga pale, pia. Na halafu Mungu … Wakati litakapopiga sehemu hiyo, Mungu atalithibitisha, "Katikati kabisa!" A-ha, yale hasa aliyosema Yeye atafanya. Hili hapa katika Maandiko, hili, "BWANA ASEMA HIVI, 'Itakuwa!'" Hili hapa. Mnaona? Haya basi.

116 Sasa, Mungu hakuwa amelifunua katika njia Yake iliyoandaliwa. Kwa hiyo walienda kufanya jambo hilo mbali na Neno Lake, na mbali na majira yake, kama tu walivyofanya sasa. Wakati mwanadamu, hata awe mwaminifu namna gani, anapojaribu kumtendea kazi nje ya njia Yake iliyoandaliwa, sikuzote wanaivuruga. Kama vile Balaamu, Balaamu alifikiri alikuwa akimtumikia Mungu.

Unafikiri Mungu hudanganya? Je! Mungu daima hubadilisha nia Yake? Vema, watu wanatenda leo kama alivyotenda. Wakati aliposema wanawake wasikate nywele zao; wanasema, "Tunaweza kuzikata, Dk. Fulani alisema tungeweza. Ndugu Fulani alisema wewe ni mtu mwenye mawazo finyu mno." A-ha, a-ha. Mnaona?

"Vema, *hili* linaweza kutukia? Jambo *hili* linatukia?"

"Naam, a-ha, Fulani alisema hivyo."

Mungu habadilishi nia Yake.

117 Mnaamini Balaamu alikuwa nabii? Biblia ilisema alikuwa nabii. Mnaamini alikuwa nabii? Sasa, kumbukeni, Balaki alimjia na kusema, "Shuka uje ukawalaani watu hawa, kwa kuwa wako kote juu ya uso wa nchi. Wao hata si madhehebu, si taifa, wao ni kundi tu lililotawanyika; nasi ni watu mashuhuri wa nchi. Sasa shuka uende kule ukawalaani watu hao, nami nitakulipa kwa ajili ya jambo hilo."

Naye Balaamu akafanya vile hasa nabii anapaswa kufanya, akasema, "Sitaenda. Ninyi ngojeni tu hapa, usiku huu, hebu nione kile Mungu anasema nifanye."

Kwa hiyo akaingia, akasema, "Bwana, kuna baadhi ya watu hapa pamoja nami waliokuja, walinitaka niende kule na kuwalaani watu wengine kule chini." Kasema, "Unataka nifanye nini juu ya jambo hilo?"

Mungu alisema, "Msiende, kwa maana hao ni watu Wangu!"

Balaamu akatoka, akasema, "Rudi nyumbani kwako. Siwezi kwenda pamoja nanyi, Mungu aliniambia nisifanye hivyo." Sasa, hilo hapo Neno la asili la Mungu: "Usiende!"

Vema, basi wakarudi, wakasema, "Unajua, askofu wako asingesikiliza."

"Vema," mfalme akasema, "nikwambie tunachofanya. Anahitaji pesa kidogo, naamini hilo lingeweza kumshawishi. Au labda nitamfanya mzee wa jimbo, labda nitampatia jambo fulani kubwa la kufanya. Huenda ningemfanya askofu, huwezi kujua ninachoweza kufanya. Hapa, nitawaambia nitafanya nini. Ninyi watu hamna elimu ya kutosha ya kumshawishi hata hivyo; *yake*, *yenu* na *hakuna*, na *chumla* na *beba* na *chukua*, si sahihi. Yeye hangewasikiliza, tutatuma kundi la watu walioelimika kule, wenye heshima zaidi."

118 Walishuka wakaenda kule, kasema, "Daktari Balaamu, *Daktari* Balaamu, salamu. Ninakuletea salamu kutoka kwa mfalme."

"Habari za asubuhi, ndugu." Mnaona?

"Sasa, Daktari Balaamu …" Na, loo, msamiati, jinsi ulivyomwagwa kweli. Kisha akasema, "Sasa, mfalme amesema ya kwamba atakuinua, na pia atakupa heshima kubwa. Na, unajua, walikupa kiasi fulani tu cha pesa kuchukua jukumu hili, lakini mfalme anasema atakizidisha mara tatu, mara nne, kama ukija tu kuzichukua." Ndipo, Balaamu, akaingiwa na hamu ya kupata faida ya haraka. Akapata mawazo ya kijinga na akachochea akili zake.

Sasa, kumbukeni, alimwita Mungu kwa hilo, ametiwa mafuta, bali alimchochea Mungu mara moja kutoka kwenye mpango wa asili. Na hivyo ndivyo Pentekoste imefanya hasa! Kupendwa na watu wengi, ninyi wa Umoja, ninyi wa Utatu, kusudi mpendwe na watu wengi mliunda madhehebu mpate kuwa tofauti, mliunda madhehebu na mmekufa! Kamwe hamtainuka tena. Lakini, mnaona, mlipaswa kudumu na Neno la Mungu la asi-… Yeye aliwavuta akawatoa kutoka hiyo Assembly kuwafanya watu, lakini mliunda madhehebu na kurudi moja kwa moja kwenye matapiko yale yale (samahani) mliyotoka kwake, takataka zile zile mlizotoka kwake "Kama mbwa anavyoenda kwenye matapiko yake na nguruwe kugaagaa matopeni mwake." Nasikitika nilisema hivyo, nisameheni, hilo halifai jukwaani hapa. Mnaona? Nilisema tu jambo hilo katika mwili. Angalia sasa ya kwamba hilo ndilo ninalomaanisha, kutapika. Nilipaswa kusema hivyo. Neno hilo lilikuwa sawa, bali lilitumiwa vibaya tu. Mnaona? Lilitumiwa vizuri, bali ni kosa tu, mwajua. Kutapika, "Kama mbwa anavyorudi kwenye matapiko yake."

119 Kama Assemblies of God, Baraza Kuu, liliunda madhehebu ya Pentekoste na kuwaingiza katika jambo

hilo kusudi wasiukubali ufunuo, je! Hamjui, Umoja, mlifanya jambo lile lile. Ungewezaje kupokea Ujumbe wa "uzao wa nyoka, usalama wa Milele," na mambo haya mengine ambayo yametokea? Ninyi mmejifunga kweli kweli kwa madhehebu hata hamtaukubali Huo kwenye mlango wenu, a-ha, a-ha, jambo lile lile alilofanya Balaamu. Lakini Mungu hakubadilisha nia Yake.

120 Kwa hiyo Balaamu aliendа pale na kusema, "Bwana, sasa angalia, kwa kweli nina nafasi sasa kuwa mtu fulani. Unajua nimekuwa mtu duni, bali nina nafasi ya kuwa mtu fulani. Unasemaje kuhusu jambo hilo sasa, Bwana?" Sasa, yeye hakupaswa kusema hivyo kamwe! Yeye alijua kile hasa Mungu alichosema ufanye!

Vivyo hivyo na kila mmoja wenu ambaye amebatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," juu ya mambo haya mengine ya Biblia yanayopaswa kuwa katika siku hii, mnajua la kufanya juu ya jambo Hilo, ni kulikubali! Unapomwona Mungu akithibitisha dhahiri "Ni Kweli," huyo ni Mungu akilifasiri Neno Lake Mwenyewe. Lakini utafanya hivyo? La, dhehebu lako halitakuacha ufanye hivyo!

121 Wengi wa wahudumu kule Tucson wanaosikiliza asubuhi hii. Ndugu Gilmore, sina neno dhidi yako; Ndugu Brock, Assembly wa Kwanza, na kanisa la kirafiki. Ninyi wanaume, nilikuwa huko wakati huo wote, hata hamkuniruhusu niingie. Mimi … Hakika, usingeweza, huwezi na kubaki jinsi ulivyo. Huwezi kukubali ufunuo, kwa sababu umefanywa dhehebu. Basi sikilizeni, kama tu vile Uzia alivyouawa kwa sababu alikuwa chini ya uvuvio huo wa uongo, vivyo hivyo na Wakristo wengi wa kweli wanapoteza ujuzi wao kule nyuma katika madhehebu hayo ya kale yaliyokufa, kwa sababu wanaweka mkono wao kwenye Sanduku wakati hawajachaguliwa kufanya hivyo. Sasa unaweza kuliamini, ama usiliamini, hiyo ni juu yako. Mungu ndiye Hakimu wako. Mungu kamwe hakurudisha nyuma Neno Lake. Yale aliyosema mara ya kwanza, Yeye huyasema kwa kila wakati.

Akamwambia Balaamu, "Usiende!"

Na halafu Balaamu akarudi, akasema, "Lakini Bwana, ningeweza kwenda?"

Sasa angalia! Mungu alisema, "Endelea!" Sasa, Yeye alimpa ruhusa ya kwenda. Kuna mapenzi ya kuruhusia ya Mungu, na si mapenzi ya asili ya Mungu. Mnaona shida aliyoipata?

122 Na mtu ye yote anayejenga kitu cho chote, madhehebu yo yote, ama cho chote nje ya Neno la Mungu, ni mchanga unaotikisika na utaanguka! Hakika kitakufa kama kitu kingine, kwa maana Neno la Mungu ni Mwili wa Bibi-arusi unaokua. Huwezi kuufanya wote kuwa ni mguu, wote ni mkono, wote ni paja. Mambo haya huja kwa wakati wake.

Na Pentekoste, uliyafanya yote kuwa kitu kimoja, kwa hiyo huwezi kukubali ufunuo mpya. Hiyo ndiyo sababu unakaa papo hapo ulipo na kufa. Linaendelea mbele. (Mengi sana, nitawachosha.) Lakini Mungu habadilishi nia Yake, uamuzi Wake wa kwanza ni sahihi kabisa. Kwa hiyo Mungu habadilishi nia Yake, Yeye anakuacha tu uendelee katika mapenzi yako ya kuruhusia. "Mungu ni Mungu mwema," kama asemavyo Oral Roberts. Yeye pia ni Mungu wa kuogofya!

123 Angalia, kama tu unavyosema, "Mungu atukuzwe, ninataka kunena kwa lugha!" Yeye atakuacha ufanye hivyo, lakini hiyo si ishara kwamba una Roho Mtakatifu.

Mnambuka vile Tomaso alivyosema, yule mwenye mashaka wa kale? "Isipokuwa niwe na ushahidi, sina budi kutia vidole vyangu katika misumari Yake, mikono Yake, na ubavuni Mwake, si—si—si—sitaamini." Sasa, haya basi, jambo lile lile.

Yesu alisema, "Haya basi, Tomaso, weka mikono yako hapa basi kama hilo ndilo unalotaka kujua." Mnaona? Mnaona? Sasa, kama unataka njia ya Thomas, endelea. Lakini Yeye alisema nini? "Ni zaidi sana vipi thawabu yao ambao hawajapata kuona na bado wanaamini."

124 Angalia, angalia, kwa kufanya jambo hili, yeye alisababisha kifo cha mtu mwaminifu; akiweka mkono wake juu ya lile sanduku wakati hakupaswa kufanya hivyo. Mtu mashuhuri, mwaminifu, alifikiri ule upako na kila kitu vilikuwa ni sawa, lakini sanduku lilikuwa likienda upande mbaya. "Ng'ombe," Biblia ilisema, "alijikunguwaa," si Walawi. Maksai alijikunguwaa na gari lilikuwa likipinduka; na mtu mwaminifu, moyo wake umejaa upendo, akaweka mkono wake kwenye sanduku hilo apate kulishikilia lisianguke, naye akapigwa akafa kwa sababu hakuna mtu angaliweza kugusa sanduku hilo ila Mlawi. Mnaona jinsi Mungu anavyoshikilia Neno Lake, jinsi anavyodumu na njia Yake, jinsi anavyoweka utaratibu Wake? Uzia alipigwa kwa ukoma. Huyu hapa Daudi, kwa jumla alisababisha mauti ya mwanadamu, na maafa makubwa; akiwa ametiwa mafuta na Roho, wote wawili, bali nje ya njia ya Mungu. Hiyo ni kweli? Yeye alikufa. Loo, lilimwogopesha Daudi hata kufa, akaita ji—jina la mahali hapo, kama vile Ndugu Jack alivyolisoma. Mnaona? Yeye alimtia alama pale.

125 Ni mara ngapi madhehebu yamefanya jambo lile lile kwa waamini wanyofu. Kanisa Katoliki, Methodisti, Baptisti, kanisa la Kristo, hata Wapentekoste, limesababisha vifo vingi vya kiroho kwa kitu kile kile. Wakati yalipokuja, na mambo haya, waliona…wala hawawezi kuendelea mbele zaidi, kwa sababu hivyo

ndivyo madhehebu yao yanavyoamini.

Angalieni leo, mikutano mikubwa, jambo lile lile. Hawafanyi kitu ila kuwafanya "watoto wa kuzimu maradufu, wabaya kuliko walivyokuwa kwanza." Wanawafanya wagumu zaidi, kwa kweli, kuja kwenye ile Kweli. Kuwa na moja ya miamsho hii mikubwa, na wote waingie, waendelee kwa muda kidogo, kisha warudi na wanaanza dhambi hii yote tena. Wanasikia juu ya ufufuo mwingine, ukisema, "Aha, nilikuwa na baadhi ya vitu hivyo, nilijaribu. Hakuna kitu kwake." Mnaona? Hawajui njia. Hawaoni.

126 Nilimsikia mwinjilisti wetu mkuu Billy Graham, aliketi asubuhi moja kwenye kiamshakinywa kama hiki, naye akasema, "Mimi …" Hapa, yeye anaandika Biblia, huko Louisville, Kentucky, kasema, "Huo hapo mfano wa Mungu." Na hiyo ni kweli, mtu huyo alisema kweli. Yeye alisema, "Nendeni … Paulo aliingia katika mji mmoja na akapata mwongofu mmoja, akarudi mwaka mmoja baadaye akakuta thelathini kutokana na huyo mwongofu." Kasema, "Lakini ninaenda katika mji fulani na kuwa na waongofu elfu thelathini, na kurudi katika miezi sita na siwezi kupata thelathini." Akasema, "Unajua kuna nini?" Kasema, "Enyi wahubiri wazembe," kasema "Mnaketi hapa huku mmeweka mguu wenu juu ya dawati na—na kuwapigia watu hawa simu badala ya kuwatembelea baada ya chakula cha jioni na kuzungumza nao."

Loo, moyo wangu ulikuwa ukiwaka moto. Nikawaza, "Ewe Mtu mashuhuri wa Mungu, ninachukia kutokubaliana nawe hapa, lakini hao wahubiri wavivu walikuwa ni akina nani kwa huyo mwongofu mmoja wa Paulo? Yale aliyofanya, yeye alimwingiza katika Neno, akamwingiza kwenye Ujumbe, akampeleka mahali alipompata Mungu; moyo wake ukawaka moto, akaiwasha nchi moto! Na jambo pekee unalofanya ni kuwaweka katika kanisa la Kibaptisti ama la Kimethodisti, ama chochote kile, si ajabu hakuna kitu cha kuwaka moto." A-ha. Naam, bwana!

127 Basi angalia kile Neno limeahidi kwa ajili ya siku hizi. Hebu na tuone kama ni Wamethodisti, Wabatisti, Wapentekoste, ama ninii, kwa ajili ya siku hizi. Sasa unaweza kwenda kusoma Maandiko yako. Chukua Maandiko haya ambayo nimekuwa nikinukuu kwako. Pia Ufunuo …

Kama ningalikuwa na wakati, ningalisoma, bali sina. Nina kama dakika kumi na mbili ama kumi na nne zaidi. Sina budi kufunga kwa wakati, saa kumi na moja, kama nikitoka vizuri.

128 Angalia Malaki 4, Ufunuo 10, Mihuri Saba. Je! Biblia haikusema … Sasa angalia! Kulikuwako na Malaika, Mjumbe kutoka juu; na mjumbe wa duniani. Na kila mjumbe alikuwa kwa ajili ya wakati wa kanisa. Yeye alisema, "Katika siku…" akinena sasa, "alikuja malaika, mjumbe" (neno malaika, ni neno la Kiingereza linalomaanisha "mjumbe"). "…alishuka kutoka Mbinguni, akaweka mguu Wake juu ya nchi na bahari, akaapa kwa Yeye aliye hai hata milele ya kwamba hakutakuwa na wakati baada ya haya." Hiyo ni kweli? Upinde wa mvua ukizunguka kichwa Chake, na mambo haya yote yakitukia tu. Malaika huyo alikuwa ni Kristo! Hakika! Lakini Yeye alisema nini? "Lakini katika siku za malaika wa saba, wakati wa saba wa kanisa."

129 Sikuzote ni katika mwisho wa wakati wa kanisa kabisa ambapo wananinii mambo sana…mambo ya kanisa yamechafuliwa sana mpaka Mungu anamtuma mjumbe, na huo ni Ujumbe kwa wakati huo wa kanisa. Ndipo wanapokea ujumbe wake, maana anaishi tu muda kidogo, na Mungu… ndipo wanachukua ujumbe wake badala ya kuuendeleza pamoja sehemu nyingine Yake, wanaunda ma—madhehebu. Ndipo wanakuja na kuunda madhehebu mengine; mjumbe mwingine, wanachukua mwingine.

Ninyi nyote mmeona katika kitabu changu, yote itachorwa katika *Nyakati Saba za Kanisa*, ambazo Yeye aliniambia; ambayo ninasimama nayo kama shahidi kwa Mungu kuhukumiwa katika Siku ya Hukumu kwa ajili Yake. Ulitoka kwa Mungu, si kwa mawazo yangu. Angalia, hapa. Niliwaza—niliwaza tofauti na hilo, kama ningekuwa na mawazo yangu mwenyewe. Kama vile Ndugu Jack alivyoniambia kuhusu Malaika pale, jinsi ambavyo "Huyo Kristo alikuwa ni mwili uliotukuzwa." Lakini haikuwa, ilikuwa inaonyesha ya kwamba Ujumbe huo ulikuwa wa kweli, Uungu Mkuu, Yeye alikuwa ni Mungu. Mnaona? Jambo lile lile tu nililokuwa nikihubiri kutoka kwa Neno. Neno daima linashuhudia Neno.

130 Sasa, upesi sasa, tunapokaribia kufunga katika dakika chache.

Sasa, Yeye alisema, "Katika siku za Ujumbe wa malaika wa saba, malaika wa duniani, wakati wa saba wa kanisa, basi siri hizi zote ambazo zimepotezwa huko nyuma katika nyakati hizi nyingine sita za kanisa zitafunuliwa wakati uo huo." Vema, hivyo ndivyo hasa wale Malaika walivyosema. Hii hapa Mihuri Saba, ama kule kufunguliwa kwa siri hizi. Nawe unajaribu kulipata mbele ya madhehebu hayo. Kinyume na kile wao … Ndugu, wanafunga kama chaza, lakini daima wamefanya hivyo. Lakini ni majira!

Ni wangapi wanaojua ya kwamba huu ni wakati wa saba wa kanisa? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!" — Mh.] Wakati wa Laodikia, ni vuguvugu ambao Mungu anatema kutoka kinywani Mwake. Nao wanamtema Mungu kutoka kinywani mwao; hakuna wakati mwingine katika Biblia ambapo Yesu alipakutwa nje akijaribu kubisha, apate kuingia. Walimfukuza, hakuna ushirikiano. Yesu ni nani? Neno! Neno lilitolewa nje. Makapi yakaitupa ngano nje! Yeye alisema, "Ninasimama mlangoni na kubisha, na mtu ye yote katika pingu hizo huko nje ataisikia Sauti Yangu." Ee Mungu, turehemu!

131 Ilikuwa ni wakati huo, wakati mtu huyo alipokufa, ambapo Daudi kwa upako aliona kosa lake. Ee Daudi, ewe mchungaji, hivi huwezi kuona kanuni zako za imani zilizokufa na madhehebu unayoshikilia? Huwezi kuona kile yanachofanya? Yanawaua akina Uzia. Kufa kiroho, halafu mnashangaa kwa nini hakuna ufufuo; kuwaachilia wanawake wenu wakate nywele zao, wajipodoe, wavae suruali fupi; mnapeleka wavulana wenu kwenye shule za kihuni, na kadhalika namna hiyo, ambapo nusu yao wanarudi nyumbani wakiwa walawiti, na kila kitu.

132 Angalia kusudi la Daudi: alikuwa akileta sanduku nyumbani mwake. Huo haukuwa mji mkuu, ambao hapakuwa mahali hapo, lilikuwa ni la Yerusalemu. Lakini Daudi alikuwa akilileta nyumbani mwake, alitaka ufufuo uwe kwenye madhehebu yake mwenyewe. "Loo, kama wewe ni Assembly, vema. Kama wewe ni wa Umoja, vema. Kama wewe ni Mpentekoste, sawa."

Kama vile mtu fulani alivyosema, kasema, "Ndugu Branham, unawezaje kuwa na mtu wa kukusikiliza?" Kasema, "Ninaweza kumwona Billy Graham, ana kila dhehebu nchini pamoja naye. Ninaweza kumwona Oral Roberts, kila Mpentekoste ananing'inia moja kwa moja kwake. Lakini," kasema "unapinga jambo hilo lote." A-ha. Kasema, "Unapataje mtu yeyote ulimwenguni?"

Nikasema, "Ni Mungu!"

"Mimi Bwana nimelipanda kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Nitalitia maji mchana na usiku isipokuwa baadhi yao walinyang'anye mkononi Mwangu,"Isaya. "Nitalitia maji, nililipanda. Niliandika majina yao kwenye kile Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwa kuchaguliwa tangu asili. Nitamwagilia maji, endelea tu kusonga mbele. Nitatoa maji, ninyi nyunyizeni tu." Sawa. Mnaona? "Nitamwagilia maji mchana na usiku isipokuwa mmoja wao atatolewa mkononi Mwangu." Haya basi.

133 Tunataka lije kwenye mji wa Daudi, mji wa Yerusalemu. Hakukuwa na mahali palipo tayari kwa ajili yake wakati huo, na ndivyo ilivyo leo. Siri hizi kuu ambazo zimefunuliwa na Mihuri Saba, hakuna mahali katika madhehebu yo yote…itakubidi kuyaacha madhehebu upate kuzikubali. Kote kote tangu Luther na kuendelea hata kwa Umoja wa Kipentekoste, hakuna mahali panapoweza kulipokea. Wala mtu hawezi kumpokea na kukaa katika madhehebu yake. Itambidi kufuata ngano la sivyo aende pamoja na kapi, achague mojawapo.

134 Kristo ndiye Sanduku letu, Neno. Wanataka madhehebu yao. Hawezi, angalia, hawezi kubebwa juu ya magari mapya ya madhehebu, Ujumbe Wake hauwezi kwenda kwenye gari la madhehebu mapya wakati linapopaswa kubebwa na kuja kwenye moyo wa nabii. Hauwezi. Yeye aliahidi, ingekuwa hivi, na hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa.

Kwa hiyo madhehebu hayatalipokea kamwe, wala hawawezi kulipokea. Nayo ni vipofu kwa hilo kama vile Wayahudi walivyokuwa walipomsulibisha Yesu msalabani, wakati Yesu aliposema, "Baba, wasamehe, hata hawajui watendalo." Usiwadharau, bali wazia tu: kwa maana vipi kama ulikuwa katika hali ile ile huku macho yako yakiwa kipofu sana hivi kwamba huwezi kuamka na kuona kile kinachoendelea?

135 Wala hawakuweza kuona ya kwamba Huyo alikuwa ni Mungu wao hasa. Wakati alipokuwa akining'inia pale msalabani, nao wakiimba Zaburi ya 22 hekaluni, umbali wa yadi mia mbili, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha? Waliichoma miguu Yangu na mikono Yangu." Mnaona? "Mifupa Yangu yote, inanikodolea macho Mimi. Mbona umeniacha?" Na hapo, Mungu yule yule waliyekuwa wamemwimbia, walikuwa vipofu vya kutosha kumfanya asulubiwe msalabani, wala hawakujua.

Sasa, hivi Biblia haisemi ya kwamba kanisa la Laodikia, ambalo linafikiri ya kwamba ni kubwa sana kwa wafuasi wake wa kimaedhehebu, litakuwa "uchi, lenye mashaka, maskini, kipofu, wala halijui"? *Kipofu* maana yake nini? *Kipofu* linamaanisha kwa kanisa hili la Laodikia kama lilivyomaanisha kwenye mwisho wa kanisa la Kiyahudi, ni kipofu kwa Kristo yeye yule waliyemweka nje, akigonga mlango, akijaribu kuingia ndani; "uchi, lenye mashaka, maskini, nyonge, kipofu, wala halijui." Ee Mungu wa rehema!

136 Kwa nini ngano haiwezi kukaa katika Uwepo wa yule Mwana kule, na kuona saa tunayoishi? Naam, Kristo ndiye Safina yetu, bali njia Yake ya asili ya kufanya jambo hilo. Basi huyu hapa … Walikuwa na Roho Wake sawa, tunajua jambo hilo. Wanamngojea Bwana, wanaona mpango Wake juu ya Neno Lake la asili katika majira Yake kuthibitishwa, hilo ndilo tunalopaswa kufanya sasa hivi. Naye ana—anafunua imani yao kwa Neno Lake, wakimwona akithibitisha kila mpango ambao Yeye aliahidi, si mipango ya kibinadamu ya madhehebu, si kufanya wafuasi kwa ajili ya safina yetu.

Wao wana safina ya Kimethodisti, safina ya Kibatisti, safina ya Kipresbiteri, kila mtu anaingia kwenye safina hii kwa ajili ya ile dhiki kuu inayokuja; "Utukufu kwa Mungu! Nilibatizwa katika safina ya Kimethodisti, ya Kipresibiteri, ya Kipentekoste." Kuna Safina moja tu, hiyo ni Yesu Kristo, Naye ni Neno!

137 Angalia, Mungu alimwambia nabii, kasema, "Kula gombo," katika Agano la Kale. Yule nabii wa Agano Jipya, Yeye alisema, "Kula hicho kitabu kidogo." Kwa nini? Kwamba nabii na Neno wangekuwa mmoja! Mnaona? Hilo ndilo Sanduku, Neno la Mungu.

Mungu ameahidi Neno Lake, jinsi litakavyotimizwa na jinsi litakavyotimia wakati Yeye alipomchagua Bibi-arusi Wake, jinsi ambavyo yangetendeka. Inatendeka moja kwa moja mbele zenu, katika Jina la Bwana, na hilo ni kwa Neno la asili! Ujumbe wa wakati wa jioni uko hapa.

Ni wangapi wanaomkumbuka Haywood alipoandika:
Kutakuwako Nuru wakati wa jioni,
Njia ya Utukufuni hakika mtaipata.

138 Naam, ile ahadi ya jioni ya Mihuri Saba, ya Ufunuo 10, Malaki 4, Luka 30 na 10. Soma Kumbukumbu la Torati 4, 4:1 na 4, halafu kifungu cha 25 na 26, uone yale aliyosema kuhusu siku hii ya mwisho. Huyu alikuwa ni Musa akiwaambia Israeli "Tiini kila Neno, usiongeze jambo moja!" Musa, nabii huyo alikuwa amepanda kule juu na kuona Neno Hilo la Mungu. Nalo liliandikwa kwa ajili yake na kuthibitishwa kwa kuandikwa na mkono wa Mungu Mwenyewe. Akasema, "Tiini kila Neno, msiongeze jambo moja Kwake wala kuondoa jambo moja Kwake." Unaweza kusoma hayo katika kifungu cha 25 na 26 cha Kumbukumbu la Torati 4.

Angalia! Usiongeze Kwake, usitoe Kwake; maana kama ukitoa, Mungu atakuondolea sehemu yako katika Kitabu cha Uzima. Na inaonyesha ya kwamba wewe hukuwa ni mbegu Yake."

139 Kumbuka! Kila kitu ambacho Mungu ametuahidi, kila kitu ambacho Mungu ametuambia, kila kitu ambacho umeambiwa katika Jina la Bwana, kimetukia! Mungu kamwe hajabatilisha ahadi moja, bali Yeye ametimiza kila ahadi aliyosema, aliyotuambia, imekuwa ni Kweli kwa miaka hii ishirini, Shreveport. Nimewahubirini katika nguvu za Mungu, na kwa heshima ya mchungaji wenu, nami nawakumbusha leo. Hata wanawake waliopita umri wa kuzaa; wanaume, watoto, mateso, kuponya, kutoa unabii, mambo ambayo yangetukia, hakuna hata moja limeshindwa! Sasa, kaa mbali na hayo madhehebu, yanakuongoza mautini.

140 Samweli alisimama siku moja, nao wakasema, "Tunataka mfalme, tunataka kuwa kama wengine wa ulimwengu."

Vema, Samweli alisema, "Msimchukue mfalme huyo. Atawachukua wana wenu, na binti zenu, naye atafanya *hili* na kufanya *lile*."

Akasema, "Naam, ninajua uko sahihi."

Lakini Samweli akasema, "Nisikilizeni. Je! Niliwahi kuchukua pesa zenu zo zote? Je! Nilipata kuwaomba nipate riziki? Je! niliwahi kuwaambia mnapaswa kunipa kiasi fulani cha mshahara kusudi niwafanyie mkutano?" Sasa amueni ninyi wenyewe, hata sasa! Mnaona? Yeye alisema, "Je! Niliwahi kuwaambia jambo lo lote katika Jina la Bwana ila lile lililotimia?" Hakuna hata jambo moja.

"Loo, naam, Samweli, kamwe hujatuomba pesa, kamwe hukutaka mambo makubwa. Samweli, hiyo ni kweli, na kila kitu ulichotuambia katika Jina la Bwana kilitimia. Lakini, Samweli, tunataka madhehebu yetu hata hivyo!"

"Basi nendeni mkayachukue. Ni juu yenu." Hiyo ni kweli.

141 Unaweza kufikiri unamtumikia Mungu, na endapo unatoka nje ya njia ya Mungu ya kufanya jambo hilo, utaendelea kuvuruga mambo, zaidi na zaidi. Ee Kanisa la Mungu aliye hai! Samahani kwa njia yangu ya Kiairishi na ucheshi wangu, lakini katika unyofu na unyenyekevu wa moyo wangu, ninyi Assemblies of God, ninyi Oneness, Wapresbiteri, Wamethodisti, cho chote mlicho, kimbieni kuokoa maisha yenu. Kumbukeni, tokeni humo.
Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka, (kujiandaa kwa ajili ya masalio hayo)
Ishara ambazo manabii walitabiri;
Siku za kimadhehebu zimehesabika zikisongwa na hofu kuu,
Rejea kwako, Ewe uliyetawanyika.
Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya wanadamu inazimia kwa hofu,
Mjazwe na Roho Wake,
Taa zenu ziwashwe na ziwe safi,
Tazama juu, ukombozi wako umekaribia.

Unaamini jambo hilo? Tuko katika wakati wa mwisho, tuko hapa. Maandishi ya mkono yako ukutani, kuja kwa pili kumekaribia, Bibi-arusi anachaguliwa, na kumwagiliwa maji, anatolewa.

142 Sasa, hilo halimaanishi kutolewa kanisani, hilo linamaanisha kuvutwa kutoka kwenye udhehebu. Huna budi kwenda kanisani, bali usijiunge na madhehebu yoyote. Yesu alienda na madhehebu yote, bali kamwe hakujiunga na moja la hayo. Wala hakuungana na hata moja la hayo, la hasha, lakini alikuwa miongoni mwao. Hapo ndipo Nuru inapaswa kutawanyika. Nawe kaa papo hapo ulipo, ukitawanya Nuru. Mnaona? Hivyo ndivyo Mungu anavyokutumia. Watu walio na njaa, hebu wajue ya kwamba Yesu Kristo ni halisi,

kama tu vile alivyokuwa jana, Yeye ni leo; na itakuwa milele.

143 Inawezekana ya kwamba mwanamume ama mwanamke kwa unyofu wote, wakijaribu wawezavyo kumtumikia Mungu, na kuichochea kwa njia mbaya. Wakiwa na upako halisi wa Roho Mtakatifu juu yao, lakini wanaichochea kinyume cha mpango wa Mungu kwa ajili ya wakati huo, na kuvuruga jambo zima. Sasa, kama unaamini hiyo ni Kweli, sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!" — Mh.] Tunalisoma tu. Wakavuruga jambo hilo lote kwa kutokuja kwa njia iliyoandaliwa na Mungu ya kufanya jambo hilo.

Hebu na tuombe.

144 Enyi kanisa, hapa na kote nchini, msikilizeni mtumishi wenu mnyenyekevu asubuhi ya leo. Utafanya hivyo? Angalieni mahali mlipokuwa miaka michache iliyopita wakati huu kwanza ulipoanza; sasa angalieni ni maigizo gani yameutumia kwa faida yao, na mamilioni na mabilioni ya dolla chungu nzima yamemiminika kwenye madhehebu. Mnaona? Tungali mbali na Neno la Mungu. Majengo na madhehebu si jinsi Mungu anavyomchochea Roho Wake. Yeye hulichochea moja kwa moja katika Neno Lake, kulifanya hai. Na kama ulikusudiwa tangu mwanzo wa dunia kwa hilo Neno, kila Neno litakuja moja kwa moja juu ya Neno. Kama vile seli ya mwanadamu haitakuwa na seli moja ya mwanadamu, na seli nyingine ni ya mbwa, na inayofuata ni seli nyingine ni ya paka; zitakuwa ni seli za binadamu. Lakini haina budi kuwa na seli kwanza. Hiyo ni kweli? Sema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema, kama ni seli ya Neno kwa kuanzia, hizo seli zingine za Neno zimechaguliwa kuufanya mwili mzima.

Msiwe watoto, isipokuwa tu katika upendo, lakini mwe watu wazima katika Roho na kuhukumu. Hukumuni kama nimewaambia Kweli au la. Hukumuni kama ni Neno la Mungu au la. Hukumuni kama ndiyo saa tunayozungumzia au la. Hukumuni kama mambo haya yameahidiwa. Sasa, je! Yamethibitishwa? Kwa mambo ambayo hakuna mwanadamu ulimwenguni angeweza kufanya jambo hilo. Lakini limekuwa jambo la kawaida sana kwetu hata tunaliacha litupite moja kwa moja. Ngojeni, kanisa, ngojeni.

145 Kama kuna mmoja hapa asubuhi ya leo ambaye hamjui Yesu Kristo, hajahesabiwa haki asubuhi ya leo, dhambi zako zote zimeondolewa kama kwamba hukuwa umetenda dhambi kamwe, na unataka kuwa namna hiyo… maana kumbuka, siku moja, huenda ikawa ni leo, labda katika dakika tano zijazo, lakini siku moja moyo huo utasimama. Na hiyo ndani ya ndani itaruka iende ikasimame mbele ya uwepo wa Mungu ikahukumiwe kulingana na kile unachofanya na Ujumbe huu asubuhi ya leo, kulingana na Ujumbe *huu* ambao unaona. Si … Si mimi, mimi ni msemaji tu. Kama vile maikrofoni hii, haiwezi kusema kitu isipokuwa ninazungumza ndani yake. Wala mimi nisingeweza kusema cho chote Mungu asipozungumza katika hilo, lakini unaona Mungu ameuthibitisha kwamba ni Kweli. Unataka kuwa Mkristo halisi.

Sasa, hatuna mahali pa wito wa madhabahuni, bali papo hapo kwenye meza unayoketi. Mahali hapa pamejaa na kusongamana, kufurika. Nisingeweza kuwaita madhabahuni, hakuna madhabahu hapa ya kuwaiteni. Lakini madhabahu iko moyoni mwako. Ruhusu ushawishi huo mdogo ya kwamba "Yesu Kristo ni halisi" usogee karibu sana leo na kuita Mwili wake mwingine kwako, upate kumweka kwenye hori la moyo wako? Kama hayuko humo, tafadhali inua mkono wako, na umpungie mkono, ukisema, "Bwana, nijaze, nijaze kwa Neno Lako na kwa Uwepo Wako, kusudi nipate kuishi Kwako"?

146 Wakati kila kichwa kimeinamishwa, kila jicho limefumbwa, kote nchini, inueni mikono yenu hapa katika wasikilizaji wanaoonekana na huko nje pia; nami nitawaombea. Hayo tu ndiyo ninayoweza kufanya, siwezi kuijaza. Mungu akubariki. Siwezi kuijaza. Mungu akubariki; na wewe. Mungu anaweza kuijaza. Mungu akubariki. Mikono inaenda juu hapa katika kusanyiko linaloonekana, kila mahali. "Ijaze. Nijaze, Ee Bwana. Nijaze." Na sasa, baada ya mimi … Asante, dada. Asante, ndugu. Mungu akubariki. Baada ya mimi … Mungu akubariki, dada mpendwa. Wewe. Baada ya … Nafikiri sasa nimewashika walio waaminifu sana, nikijaribu kuwa, ninataka kuinua mikono yangu pamoja nanyi.

Ee Bwana, usiniruhusu kamwe kusimama. Daima, Bwana, hebu nisiishie katika jambo moja, hebu niendelee tu, Bwana, mpaka nitakapomaliza kila kitu ulichonichagulia kufanya. Bila kujali gharama, haidhuru gharama, haidhuru kukosolewa, jinsi msalaba ulivyo mgumu, nitaukumbuka msalaba ulioubeba.

Kwa hiyo nitabeba huu msalaba uliowekwa wakfu
Hadi kifo kiniweke huru;
Kisha nienda nyumbani, kuvaa taji,
Kuna taji kwa ajili yangu.
Lazima Yesu abebe msalaba Mwenyewe,
Na ulimwengu wote uwe huru?
Hapana, kuna msalaba kwa ajili ya kila mmoja wa wanawe,
Kuna msalaba kwa ajili yangu.

147 Mungu mpenzi, Neno limetoka. Haliwezi kurudi bure, litapata mahali Pake mahali fulani. Kama mbegu tayari imepandwa, litainyunyizia maji mpaka ikue. Wala hakuna mtu anayeweza kuitoa katika mkono Wako, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, hakuna mtu anayeweza kuwatoa kwenye mkono Wangu. Baba amenipa hao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu"; wakati mipango yote ilipoandaliwa, basi, Yesu apewa Kanisa Lake, Bibi-arusi Wake.

Ndoa ya bandia ya ulimwengu, kwa madhehebu haya. Ulikuja na ukafa ulimwenguni, ukamkomboa, ukamhesabia haki, Yeye hakufanya hivyo mara ya kwanza. Alikuwa amenaswa ndani yake, kipofu. Na kama vile wimbo unavyosema:

Nilikuwa nimepotea wakati mmoja na sasa nimepatikana,
Nilikuwa katika Laodikia wakati mmoja, kipofu, lakini sasa naona.
Na neema ndiyo iliyofundisha moyo wangu kuogopa,
Ilikuwa ni neema iliyoondoa woga wangu;
Ni ya thamani iliyoje ile neema iliyoonekana
Ile saa nilioamini kwanza.

Na yale maji ya Mungu yalidondoka juu ya nafsi yangu. Nilikuwa nikiugua.

148 Mungu, kwenye madhabahu hii ndogo ya kila moyo uliopo hapa na kote nchini, naomba maji yanayotoka chini ya madhabahu ya Mungu na yabubujike asubuhi hii juu ya Kanisa Lako; na kulimwagilia maji, Bwana, kwa maana majira yanakaribia kwisha. Lipe Uzima, Maji ya Uzima, lipate kukaa katika Uwepo wa yule Mwana kusudi liivishwe kwa ajili ya ghala Lako kuu.

Baba, ninawaombea. Lakini shina halina budi kukauka, kwa hiyo siwezi kuliombea; halina budi kufa, kwa hiyo limekufa. Lakini ninaomba kwa ajili ya ngano, Bwana, ambayo inaumbika katika Mwili wa Kristo. Tujalie, Bwana, ya kwamba maji baridi ya Mungu yatadumisha mashavu yake masafi na maji ya furaha na ufahamu mpaka kivuna nafaka kitakapokuja kuipeleka Nyumbani. Katika Jina la Yesu, ninayakabidhi yote Kwako, Bwana; matokeo ni Yako. Amina.

149 [Dada fulani katika kusanyiko anatoa ujumbe — Mh.] Amina.

Kwa hiyo Baba, Mungu, tunakushukuru. Na, Baba, tunamwombea dada yetu mdogo, mjakazi hapa, kwa ajili ya nguvu zake. Ninafikiria wakati ambao wakati ni—nilipotembea mbele yake, jinsi ambavyo Roho alikuja juu yake na kutoa ujumbe ule ule ambao Malaika wa Bwana alitoa Mtoni siku hiyo: "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Bwana Yesu, wewe umetumwa kutangulia kuja mara ya pili."

Tukiona likiumbika sasa katika sehemu ya ngano, Mungu, tunakushukuru kwa kila kitu ambacho umefanya. Mioyo yetu imejaa kupita kiasi. Ninajisikia nimejaa sana, Bwana, sijui jinsi ya kusema jambo lingine lo lote. Lakini asante Baba, tena, kwa yote uliyotufanyia. Kupitia Jina la Yesu Kristo.

Nampenda, …

Hebu na tumwimbie tu, sasa. Kumbuka, Yeye yuko hapa.

Kwa sababu alinipenda kwanza,
Na akanunua wokovu wangu
Kwenye mti wa Kalvari.

150 Je, hilo linawafanya mjisikie duni sana, duni sana? Mmemwaga yote, mkiwa tayari kwa Roho, mnaona.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Usitamani utajiri wa bure wa ulimwengu huu,
Unaooza upesi sana,
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele, (hakuna madhehebu, sasa)
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

151 Ni wangapi wanaojaribu kufanya jambo hilo? Inua mkono wako. Sasa nyosha mkono upande wa pili wa meza, wekeaneni mikono, namna *hii*, pamoja. Unaweza kuketi, hilo ni sawa, ama cho chote unachotaka kufanya. Sikilizeni kwa makini. Hebu na tuuimbe pamoja sasa. Hii inawakilisha mnyororo wetu usiovunjwa wa upendo wa Mungu. Tunashikana mikono kwa sababu tunamwamini Mungu. Tunagusana kwa sababu sisi ni ndugu na dada, Roho yule yule anayetetemeka, Neno la Milele la Mungu linalokaa mioyoni mwetu likidhihirishwa.

Wakati safari yetu ikishakamilika,
Ikiwa ulikuwa mkweli kwa Mungu,
Nyumba kwetu kwenye Utukufuni kuzuri na kunang'aa,
Nafsi zetu zilizofurahi zitaona!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika! (Roho wa Bwana!)
Mshikilie Mungu …

Weka tu nia yako Kwake, mnaona. Hii ndio aina ya mikutano ambayo hatuna budi kuhudhuria katika siku zijazo.

… Mkono usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele- …

Neno ndilo jambo pekee lililopo ni la Milele.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Usitamani umaarufu wa bure wa ulimwengu huu, elimu,
Huo unaoza haraka, (Liangalie hilo leo, kile limefanya.)
Tafuta kupata hazina ya mbinguni,
Hivyo havitapita kamwe!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

152 [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine. Ndugu Branham anaanza kuuvumisha *Shikilia Mkono wa Mungu usiobadilika.* Dada mwingine anatoa tafsiri — Mh.]

Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Bwana. Tunapoketi katika wakati huu wenye uchaji, karibu kama kwenye mazishi, kwa maana tunakabili mazishi ya ulimwengu uliokufa, ulimwengu unaokufa; kanisa linalokufa, lililokufa.

Ee Mungu, kukusanya ngano Yako upesi, Baba. Njoo upesi, Bwana Yesu.

Wabariki watu Wako, Baba, ulete unyofu na kilindi kwenye mioyo ya watu. Jalia tutoke kwenye hizo dansi dhaifu na batili, tutulie kwenye utajiri mkubwa wa kina cha asali ya Mungu. Jalia hilo, Bwana. Weka mioyo yetu imara kwa upendo na unyofu.

Wabariki watu Wako kila mahali, Baba. Tunapoondoka mahali hapa na tuende katika Jina la Bwana Yesu kunena yale yaliyo ya uaminifu, yale yaliyo Kweli, yale yaliyo sahihi, jalia tujiepushe na yaliyo mabaya, Bwana. Wakati mtu anapoanza kutudanganya, na tumwonyeshe kisogo upesi, tukatae mizaha yote michafu, mibaya na mambo ya ulimwengu, na tuyape kisogo tu na kujiondokea. Tusaidie, Mungu mpendwa. Tufinyange, tutengeneze, tuvunje, na utufanye kuwa mfano wa wana na binti za Mungu tupate kutenda kazi kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Tunajikabidhi Kwako, huku mikono yetu ikiwa katika kila mmoja, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Hebu na tusimame. Ndugu Noel.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7